# Nipashe

Jumatano Agosti 28, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581782

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



MIGOMO NA MAANDAMANO SASA MAHAKAMA KUWAJIBISHA VIGOGO

siasa

Nipashe

ACT Wazalendo imerejea na zigo la kero za wananchi mikoani

MITANDAO YA KIJAMII ILIVYO TISHIO KUFIKIA 50/50

UKURASA 11

**Samia** aleleza umuhimu wa mageuzi ya kikatiba AU UKURASA 2



**Janabi** aonya hatari unywaji juisi ya matunda ya kukamuliwa UKURASA 3



**PM** ahimiza vyuo kuzalisha wahitimu wenye maarifa ya juu UKURASA 5


Angelina Mabula

Dk. Tulia Ackson

# Sakata wodi lazua kizaazaa bungeni

• **Yaelezwa** kulaza wanaume, wanawake na watoto kwa pamoja, Spika ataka ukweli ujulikane... *Endelea uk. 3*



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiwa na mwenyeji wake, Rais wa Kenya Dk. William Ruto (wa tatu kulia) pamoja na viongozi wengine, wakati wa hafla ya uzinduzi wa Kampeni ya Raila Odinga, Waziri Mkuu mstaafu wa Kenya anayewania nafasi ya Mwenyekiti Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AU), Ikulu ya Nairobi, jana. **Habari Uk. 2. PICHA: IKULU**

## Aliyenaswa wizi mtoto adaiwa kutaka kulipwa milioni 50/-

UKURASA 2

## Mashirika 40 tegemezi sasa kupigwa panga

UKURASA 7

**MICHEZO** YANGA YAMWEKEA NGUMU RASMI MZIZE UK.24 **MAONI,** UK.6

# Samia aeleza umuhimu AU kuzingatia mageuzi kikatiba

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema nchi za Afrika zina wajibu wa kuhakikisha Umoja wa Afrika (AU), unaendelea kushikamana kwa kuzingatia malengo makuu na muhimu yaliyowekwa ikiwamo kuzingatia mageuzi ya kikatiba.

Pia, nchi hizo zitambue zinawajibu wa kuimarisha uwajibikaji na kuweka silaha chini na kuupa nafasi umoja huo kutimiza malengo iliyojiwekea ikiwamo ajenda ya maendeleo.

Aliyasema hayo jana akiwa Nairobi, nchini Kenya katika hafla ya uzinduzi wa kampeni ya Raila Odinga, Waziri Mkuu mstaafu wa Kenya, anayewania nafasi ya Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AU).

"Pamoja na hatua zilizofikiwa na umoja huu, kuna haja ya kuyafikia malengo makuu kwa kuhakikisha, sauti zetu, sauti za Waafrika zinasikika kwenye mijadala ya kidunia, hasa katika mabadiliko ya tabianchi kuingia kwenye nishati safi.

Kufikia maendeleo ya Akili Mnemba (AI) duniani. Hii ina maana kwamba Serikali ya Tanzania inamthibitisha Raila Odinga, kuwania nafasi ya Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AU). Tanzania inamfahamu Odinga kwamba ni Mwafrika kiongozi anayeamini katika ushirikiano kivitendo," alisema Rais Samia.

Alisema, Raila mwenye taaluma ya uhandisi anafahamu AU inahitaji zaidi miundombinu ili kuondokana na pengo lilimo kwenye sekta hiyo ili kufikia Afrika imara na yenye uwezo.

"Odinga anaweza kusimama imara katika kuhakikisha kipaumbele cha maendeleo kwa Afrika kinazingatiwa. Tanzania inawahakikishia kwamba inaungana na Wakenya, kumuunga mkono Odinga kuwania nafasi hiyo...baba anatosha, achaguliwe," alisema Samia.

Rais wa Uganda, Yoweri Museveni alisema kwamba tatizo kubwau liliopo miongoni mwa nchi za kiafrika ni umaskini, unaohitaji kupatiwa ufumbuzi kwa kuhakikisha kuna huduma muhimu bora za kijamii.

"Tunahitaji madaktari wa kiuchumi kwenye jamii na kuiangalia jamii zetu Afrika utajiuliza nini tatizo, makabila, dini zipo. Tukaja tukabaini ugonjwa mkubwa ni ustawi duni kwenye jamii, umaskini.

"Watu wanahitaji chakula, malazi, elimu na kwa namna gani watavipata? Unahitajika ustawi wa kijamii. Watu kama wanazalisha mali bila hesabu, wanashindwa kufanya uchambuzi watashindwa kuondokana na umaskini," alisema Museveni.

Alisema katika yote kikubwa kinachohitajika ni uzalendo kutoka kwa wananchi wa bara hilo, kwa kununua bidhaa zinazolishwa nchini mwao ili kuinua kiwango cha soko na uchumi wa ndani.

Hafla hiyo imehudhuriwa pia na Rais Museveni; Rais wa Jamhuri ya Sudan Kusini, Salva Kiir Mayardit; Waziri Mkuu wa Burundi, Gervais Ndirakobuca na viongozi wengine.


Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Mwanga Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania

Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA


VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | NYARAKA YA UMILIKI NA SEHEMU | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | JACQUELINE TESHA AKIWA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU CHIEDRICK KOMBA JARIBUNI | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - TABATA KINYEREZI | J&J RECOVERIES | 10/09/2024 |
| 2 | ADIN HODLAM MSANYA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – KILOSA MOROGORO | J&J RECOVERIES | 10/09/2024 |
| 3 | SYLIVIA BIRANE BALWIRE | GARI | T 346 DKM –TOYOTA FORTUNER | JODAC PROFESSIONAL LTD | 12/09/2024 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika vyombo husika vya Serikali.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson akimwapisha Hamza Johari kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), wakati wa mkutano wa 16 wa Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Aliyenaswa tuhuma kuiba mtoto adaiwa kutaka alipwe milioni 50/-

**Na Romana Mallya**

MKAZI wa Mikwambe, wilayani Kigamboni, mkoani Dar es Salaam, Zakia Timu (26), anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumwiba mtoto Zulkaiya Ndambwe (4) kama 'dili' la kujipatia Sh. milioni 50.

Mwanamke huyo baada ya kuhojiwa inadaiwa amekiri kumwiba mtoto huyo baada ya kupata taarifa ya mtu aliyekuwa anatafuta mtoto asiye na wazazi na anaishi katika mazingira magumu ili aweze kufuata taratibu za kumwasili.

Shaka iliyojitokeza ni pale mwanamke huyo kudaiwa kutaka anayehitaji kuasili mtoto amjengee nyumba ya vyumba vitatu au kupewa Sh. milioni 50 kwa ajili ya mtoto huyo.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) David Misime alisema jana kuwa kutokana na kinachodaiwa tamaa za mwanamke huyo, aliona amepata 'dili' na kwenda kuiba mtoto huyo.

DCP Misime alisema kuwa Agosti 8 mwaka huu, ilitolewa taarifa ya polisi kuwa katika Kijiji cha Jaribu Mpakani, wilayani Kibiti, Mkoa wa Kipolisi Rufiji, mtoto huyo amepotea.

"Taarifa za kupotea mtoto huyo zilisambaa pia katika mitandao ya kijamii na baadhi ya watu walitoa maoni mbalimbali, matamshi na maneno chanya na hasi.

"Uchunguzi wa awali ulibainisha kuwa mtoto huyo alichukuliwa na mwanamke mmoja mweupe alipokuwa anacheza na watoto wenzake," alisema.

DCP Misime alisema Jeshi la Polisi lilipokea taarifa nyingi na baada ya kuzichambua kwa kina, nyingi zilibainika si za kweli, zingine zilikuwa ni za kutaka kulipiza kisasi na nyingine kutaka kusambaratisha familia.

Alisema kwa vile Jeshi la Polisi lilisambaza taarifa za kupotea kwa mtoto huyo maeneo mbalimbali, Agosti 23 mwaka huu, zilipokewa taarifa kutoka kwa raia wema kuwa mtoto huyo amepatikana huko Mikwambe, akiwa na mwanamke huyo.

"Amekiri kumwiba mtoto huyo na kutokana na kukutwa naye na kwa kukiri kwake, Jeshi la Polisi linaendelea kumshikilikia ili kukamilisha uchunguzi," alisema.

Alisema kilichomsukuma kufanya tukio hilo ni baada ya kupata taarifa ya mtu huyo anayetaka kumwasili mtoto.

DCP Misime alisema alipoambiwa waanze kufuatilia taratibu na kutakiwa alete ndugu wengine, vyeti na waende kwa kiongozi wa Serikali za Mitaa kwa utambuzi, mwanamke huyo alianza kusita na kushindwa kutekeleza masharti hayo.

"Ndipo shaka ikaanza na kusababisha kutiliwa shaka. Shaka nyingine ilijitokeza pale alipoanza kudai ajengewe nyumba ya vyumba vitatu au apewe Sh. milioni 50," alisema.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Jeshi la Polisi kupitia makamanda wake wa mikoa ya Shinyanga na Mwanza, lilieleza kuwa matukio mengi ya wizi wa watoto yanatokana na wanaoiba kutokuwa na uwezo wa kuzaa.

HABARI KITAIFA

# Prof. Janabi: Juisi ya kukamua hatari

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi amesema unywaji juisi iliyokamuliwa kwa matunda halisi, unaweza kuwa hatari kiafya kutokana na kiwango cha matunda kinachotumika kuwa kwa wingi.

Anasema kiafya tunda linapaswa kuliwa kama lilivyo kabla ya kulichakata ama kulikamua na kuwa juisi.

Anasema kula matunda badala ya juisi kunasaidia mlaji kubaini kiwango na idadi ya matunda aliyokula.

Prof. Janabi, ambaye pia ni Mhadhiri Mshiriki wa Chuo Kikuu cha Magonjwa ya Moyo cha Marekani (FACC), anatoa 'darasa' hilo katika kitabu chake cha 'Mtindo wa Maisha na Afya Yako'.

"Ni vyema kula tunda lilivyo kuliko kukamua juisi. Kwa mfano, ili upate glasi moja ya juisi ya chungwa, unahitaji machungwa matano.

"Ukinywa glasi tatu kwa siku, yaani asubuhi, mchana na jioni, maana yake itakuwa umekula machungwa 15 na kwa siku 10 ni sawa machungwa 150 na kwa mwezi ni machungwa 450.

"Hicho ni kiasi kikubwa sana ambacho kinaweza kuleta shida mwilini kutokana na kiwango chake cha sukari," anasema Prof. Janabi ambaye pia ni bingwa wa magonjwa ya moyo.

Anasema tatizo la magonjwa yasiyoambukiza (NCD), ni janga na chimbuko lake ni tabia ya ulaji chakula usio sahihi. "Kwa maana hiyo, njia ya kwanza kushughulika na janga hili



Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Jaji Jacobs Mwambegele (kushoto), akizungumza wakati akifungua mafunzo ya siku mbili kwa Waratibu wa Uandikishaji wa mkoa, Maofisa Waandikishaji, Maofisa Waandikishaji Wasaidizi ngazi ya Jimbo, Maofisa Uchaguzi, Maofisa Ugavi na Maofisa TEHAMA wa Halmashauri, mjini Musoma, mkoani Mara juzi. **PICHA: INEC**

# Serikali yatoa kibali ajira mpya 47,404

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema katika mwaka wa fedha 2023/24, imetoa kibali cha nafasi 47,404 za ajira mpya kwa waajiri wote ambazo kila mwajiri katika jimbo amepata nafasi kwa kuzingatia Ikama ya watumishi katika maeneo hayo.

Aidha, katika kutekeleza kibali hicho, serikali kupitia Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imetangaza nafasi katika kada za Elimu na Afya kimkoa na usaili utafanyika katika ngazi ya mkoa.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimeti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, alisema hayo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Nachingwea, Amandus Chinguile (CCM).

Mbunge huyo alihoji kuwa serikali haioni haja ya kuanzisha mfumo utakaowezesha kupata idadi sawa ya nafasi za ajira katika kila jimbo kuliko mfumo wa sasa.

Akijibu swali hilo Sangu alisema kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2008, toleo la pili, aya ya 4.2, nafasi za ajira hutolewa kwa ushindani na kwa kuzingatia sifa stahiki kwa mujibu wa Miundo ya Maendeleo ya Utumishi ya kada husika.

"Vile vile, nafasi wazi za ajira hutolewa kwa kuzingatia ikama ya watumishi katika taasisi husika ambayo inajumuisha mahitaji halisi yaliyopo katika taasisi husika," alisema.

Alisema kwa mujibu wa hati idhini inayoanzisha kila taasisi, mahitaji ya watumishi ya taasisi moja hutofautiana na nyingine kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ukubwa na wingi wa majukumu.

Vile vile, alisema idadi ya taasisi za umma zinatofautiana kwa kila jimbo.

"Kwa msingi huo, idadi ya nafasi za ajira hutofautiana kati ya jimbo moja na jingine," alisema.

"Kutokana na maelezo hayo, katika mwaka wa fedha 2023/2024, serikali imetoa kibali cha nafasi 47,404 za ajira mpya kwa waajiri wote, kila mwajiri katika kila jimbo amepata nafasi kwa kuzingatia Ikama ya Watumishi katika maeneo hayo," alisema.

# Sakata wodi lazua kizaazaa bungeni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MBUNGE wa Ilemela (CCM), Dk. Angelina Mabula, ameibua sakata jipya bungeni:

Katika siku ya kwanza ya mkutano wa Bunge jana, alisema Kituo cha Afya Sangabuye, Manispaa ya Ilemela, mkoani Mwanza kina wodi moja inayotumiwa na wanaume, wanawake na watoto.

Kutokana na hoja hiyo ya mbunge, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ameelekeza Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) itafute taarifa kwa kina kuhusu suala hilo na kutolea ufafanuzi bungeni - watu hao wanalalaje katika wodi moja ili jambo hilo likae vizuri katika taarifa za Bunge.

Akiuliza swali la nyongeza bungeni jana, mbunge huyo alisema kituo hicho kimetokana na kupandishwa hadhi kutoka zahanati na kuwa kituo cha afya mwaka 1999, lakini hadi sasa kina wodi moja inayotumiwa na wanawake, wanaume na watoto na kuhoji ni lini serikali itakamilisha majengo ya kituo hicho pamoja na kujenga uzio.

"Katika kituo hicho, kitanda kimoja unakuta amelazwa mwanamke na kinachofuata, mwanamume na kingine mwanamke ana mtoto, na ni kutoka mwaka 1999 miundombinu haijakamilika," alisema.

Kabla ya kumkaribisha Naibu Waziri Ofisi ya Rais Dk. Festo Dugange, Spika wa Bunge Dk. Tulia Ackson alionesha kushtushwa na jambo hilo na kumhoji mbunge Mabula:

"Mheshimiwa Angelina Mabula; watoto, wanawake na wanaume wanalazwa katika wodi moja?"

Mbunge huyo akajibu, "Kweli Mweshimiwa Spika". Spika Tulia akauliza tena, "Wanawezaje kwa wodi moja, ninapata shaka, yaani wameweka mapazia au nini?"

Akitoa ufafanuzi kuhusu hilo, Mbunge Mabula alisema, "Katika kituo hicho cha afya unaweza ukakuta kitanda kimoja amelazwa mwanamke, kitanda kinachofuata kuna mwanamume na kingine kuna mwanamke mwenye mtoto, ndani ya wodi moja na ni tangu 1999 miundombinu hiyo haijakamilika."

Katika majibu yake, Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Dk. Dugange, alisema kuwa kwa mujibu wa utaratibu na Sera ya Afya, hairuhusiwi kulaza wagonjwa wa jinsia tofauti katika wodi moja.

"Kwa taarifa hii, TAMISEMI tunaipokea kwamba kuna tatizo katika uongozi wa hospitali hiyo na manispaa yenyewe.

"Ninaomba Mheshimiwa Spika nichukue hoja hii nimwelekeze Mkurugenzi wa Manispaa leo (jana) hii afike pale mara moja na atupe taarifa rasmi TAMISEMI, ili kuona namna nzuri ya kutoa huduma kwa wagonjwa wanaolazwa kwa kuwa haikubaliki kulaza wanawake na wanaume wodi moja," alisema.

Dk. Dugange pia alimwagiza Mkurugenzi wa manispaa hiyo kupitia mapato ya ndani kuanza ujenzi wakati TAMISEMI ikitafuta fedha kwa ajili ya kuwaunga mkono.

Awali katika swali la msingi, Mbunge wa Korogwe Mjini (CCM), Dk. Alfred Kimea, alihoji lini Kituo cha Afya Mgombezi kitapatiwa fedha iliyobaki Sh. milioni 250 ili kumalizia ujenzi wake.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange alisema katika mwaka wa fedha 2021/22, serikali iliipatia Halmashauri ya Mji wa Korogwe, Sh. milioni 250 kwa ajili ya kuipandisha hadhi Zahanati ya Mgombezi kuwa kituo cha afya.

"Fedha hizo zimejenga wodi ya wazazi na jengo la upasuaji ambapo, jengo la wazazi tayari limekamilika na linatumika. Jengo la upasuaji lipo katika hatua ya umaliziaji ambapo zinahitajika Sh. milioni 36 kulikamilisha," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema kuwa katika mwaka wa fedha 2025/26, serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Mji wa Korogwe itakitengea Sh. milioni 36 kwa ajili ya

ukamilishaji jengo la upasuaji na serikali itatenga Sh. milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu iliyosalia.

**TANGAZO**

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## PRESIDENT'S OFFICE-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

## SERENGETI DISTRICT COUNCIL

HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI

## STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE FOR THE FINANCIAL YEAR ENDED 30 JUNE 2023

*Classification of Expenses by Nature*

| | Note | 2023 TZS | 2022 TZS |
|---|---|---|---|
| **REVENUE** | | | |
| **Revenue** | | | |
| Revenue from Exchange Transactions | 17 | 275,226,811 | 178,960,336 |
| Levies | 18 | 1,370,483,899 | 755,840,951 |
| Fees, Fines, Penalties and Forfeits | 19 | 641,702,521 | 260,304,484 |
| Social Contributions (Revenue) | 20 | 231,971,093 | 170,644,080 |
| External Assistance | 25 | 888,251,204 | 0 |
| Other Revenue | 31 | 1,679,494,378 | 1,183,282,510 |
| Subvention from other Government entities | 32 | 34,045,775,247 | 35,118,188,076 |
| **TOTAL REVENUE** | | **39,132,905,153** | **37,667,220,437** |
| **EXPENSES AND TRANSFERS** | | | |
| **Expenses** | | | |
| Wages, Salaries and Employee Benefits | 34 | 26,306,015,807 | 26,651,424,924 |
| Use of Goods and Service | 35 | 1,667,715,919 | 3,902,863,129 |
| Maintenance Expenses | 36 | 144,547,698 | 179,598,204 |
| Other Expenses | 52 | 59,207,900 | 41,530,668 |
| Social Benefits | 56 | 840,778,062 | 1,101,995,899 |
| Depreciation of Property, Plant and Equipment | 77 | 805,228,731 | 441,614,315 |
| **Total Expenses** | | **29,823,494,117** | **32,319,027,139** |
| **Transfer** | | | |
| Other Transfers | 60 | 230,806,633 | 142,094,139 |
| **Total Transfer** | | **230,806,633** | **142,094,139** |
| **TOTAL EXPENSES AND TRANSFERS** | | **30,054,300,750** | **32,461,121,278** |
| **Surplus / (Deficit)** | | **9,078,604,404** | **5,206,099,157** |

Council Director — Date: 23.03.2024

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR SERENGETI DISTRICT COUNCIL

**STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30 JUNE 2023**

| | Note | 2023 TZS | 2022 TZS |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current Asset** | | | |
| Cash and Cash Equivalents | 62 | 2,735,451,511 | 705,579,697 |
| Receivables | 67 | 517,978,262 | 720,093,293 |
| Prepayments | 69 | 10,597,665 | 10,597,665 |
| Inventories | 70 | 708,855,551 | 207,467,074 |
| Other Financial Assets | 71 | 39,662,200 | 39,662,200 |
| **Total Current Asset** | | **4,012,545,189** | **1,683,399,929** |
| **Non-Current Asset** | | | |
| Property, Plant and Equipment | 77 | 20,891,437,212 | 16,620,859,882 |
| Work In Progress | 82 | 2,655,658,834 | 1,345,117,367 |
| **Total Non-Current Asset** | | **23,547,096,046** | **17,965,977,249** |
| **TOTAL ASSETS** | | **27,559,641,235** | **19,649,377,178** |
| **LIABILITIES** | | | |
| **Current Liabilities** | | | |
| Payables and Accruals | 89 | 2,204,596,213 | 3,685,065,003 |
| Deferred Income | 93 | 535,446,038 | 546,569,653 |
| Deposits | 94 | 489,258,679 | 166,006,620 |
| **Total Current Liabilities** | | **3,229,300,930** | **4,397,641,276** |
| **TOTAL LIABILITIES** | | **3,229,300,930** | **4,397,641,276** |
| **Net Assets** | | **24,330,340,305** | **15,251,735,902** |
| **NET ASSETS/EQUITY** | | | |
| **Capital Contributed by:** | | | |
| Other Reserves | | 39,662,200 | 39,662,200 |
| Taxpayers/Share Capital | | 0 | 0 |
| Accumulated Surpluses / (Deficits) | | 24,290,678,105 | 15,212,073,702 |
| **TOTAL NET ASSETS/EQUITY** | | **24,330,340,305** | **15,251,735,902** |

Council Director — Date: 23.03.2024

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR SERENGETI DISTRICT COUNCIL MUGUMU / SERENGETI

| | 2023 TZS | 2022 TZS |
|---|---|---|
| **CASH FLOW FROM OPERATING ACTIVITIES** | | |
| **RECEIPTS** | | |
| Tax Revenue | 0 | 0 |
| Subvention from other Government entities | 33,217,338,333 | 32,941,999,964 |
| Social Contributions (Revenue) | 231,971,093 | 170,644,080 |
| Revenue from Exchange Transactions | 275,226,811 | 178,960,336 |
| Receipt from Repayment of Advances/Loan made to other parties | 0 | 0 |
| Other Revenue | 1,899,907,526 | 1,118,058,832 |
| Levies | 1,370,483,899 | 755,840,951 |
| Increase in Deposit | 323,252,059 | 0 |
| Fees, Fines, Penalties and Forfeits | 641,702,521 | 260,304,484 |
| External Assistance | 888,251,204 | 0 |
| **Total Receipts** | **38,848,133,446** | **35,425,808,647** |
| **PAYMENTS** | | |
| Wages, Salaries and Employee Benefits | 27,675,490,107 | 26,468,130,234 |
| Use of Goods and Service | 1,653,797,519 | 3,456,386,525 |
| Social Benefits | 840,778,062 | 1,101,995,899 |
| Other Transfers | 258,192,820 | 118,700,000 |
| Other Expenses | 59,207,900 | 41,530,669 |
| Maintenance Expenses | 144,547,698 | 179,598,205 |
| Grants and Transfers | 0 | 0 |
| Decrease in Deposit | 0 | 398,703,900 |
| **Total Payments** | **30,632,014,106** | **31,765,045,432** |
| **NET CASH FLOW FROM OPERATING ACTIVITIES** | 8,216,119,343 | 3,660,763,214 |
| **CASH FLOW FROM INVESTING ACTIVITIES** | | |
| **Investing Activities** | | |
| Payment for Work in Progress | (1,310,541,467) | (1,345,117,367) |
| Acquisition of Property, Plant and Equipment | (4,875,706,061) | (3,644,102,868) |
| Acquisition of Biological Assets | 0 | 0 |
| **Total Investing Activities** | **(6,186,247,528)** | **(4,989,220,235)** |
| **NET CASH FLOW FROM INVESTING ACTIVITIES** | **(6,186,247,528)** | **(4,989,220,235)** |
| Net Increase | 2,029,871,814 | (1,328,457,021) |
| Cash Surrendered to Holding Account | 0 | 0 |
| Cash and cash equivalent at beginning of period | 705,579,697 | 2,034,036,718 |
| Cash and cash equivalent at end of period | 2,735,451,511 | 705,579,697 |

Council Director — Date: 23.03.2024

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR SERENGETI DISTRICT COUNCIL

33

### 1.0 INDEPENDENT REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL

Hon. Chairperson of the Council,
Serengeti District Council,
P.O. Box 176,
MUGUMU.

### 1.1 REPORT ON THE AUDIT OF FINANCIAL STATEMENTS

**Qualified Opinion**

I have audited the financial statements of Serengeti District Council, which comprise the statement of financial position as at 30 June 2023, the statement of financial performance, statement of changes in net assets, cash flow statement and the statement of comparison of budget and actual amounts for the year then ended, as well as the notes to the financial statements, including a summary of significant accounting policies.

In my opinion, except for the effects of the matters described in the basis for qualified opinion section of my report, the accompanying financial statements present fairly in all material respects, the financial position of Serengeti District Council as at 30 June 2023, and its financial performance and its cash flows for the year then ended in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) Accrual basis of accounting and the manner required by the Local Government Finances Act, Cap. 290.

Charles E. Kichere
Controller and Auditor General,
Dodoma, United Republic of Tanzania.
March 2024

HABARI KITAIFA

# Kesi kupinga TAMISEMI kusimamia uchaguzi wa mitaa kuanza kuunguruma

**Na Grace Mwakalinga**

KESI ya kupinga Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa uliopangwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu, kuanza kusikilizwa leo.

Kesi hiyo iliyofunguliwa na Watanzania watatu, Bob Wangwe, Dk. Ananilea Nkya na Bubelwa Kaiza, itasikilizwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam mbele ya Jaji Wilfred Dynsobera

Msingi wa pingamizi hilo ni kuiomba mahakama kuiondoa TAMISEMI kusimamia uchaguzi huo kwa kuwa Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ya mwaka 2024 na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara ya 76 (6) (e) inaitambua tume kusimamia uchaguzi.

Wakizungumza jana na waandishi wa habari, walalamikaji hao walisema kitendo cha TAMISEMI kusimamia uchaguzi ni batili kwa kuwa inapoka haki, uwazi na kusababisha michakato kutoaminika.

Dk. Nkya alisema kwa mujibu wa katiba, wanaona ni kinyume cha sheria za nchi iwapo TAMISEMI itasimamia uchaguzi wa serikali za vijiji, kamati za mitaa na wenyeviti wa vitongoji.

Alifafanua kuwa kifungu cha 10 (1) (c) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi namba 2 ya mwaka 2024, kinatoa wajibu na mamlaka ya kusimamia uchaguzi wa serikali za vijiji, kamati za mitaa na wenyeviti wa vitongoji kwa tume na si TAMISEMI.

"Tumefungua shauri hili kwa kutambua kwamba raia ndio mamlaka ya nchi kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania Ibara ya 8 (1) (a) ambayo inaeleza wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi," alisema.

Dk. Nkya alisema msingi wa kisheria wa shauri hilo ni kuhoji TAMISEMI kusimamia uchaguzi kunaleta hatari ya utoaji wa haki na uwazi wa mchakato wa uchaguzi, hivyo uamuzi wa kupinga, unalenga kulinda haki ya kikatiba ya raia wa Tanzania kushiriki mchakato kidemokrasia.

Wangwe alisema kwa mujibu wa Ibara ya 26 (2) ya Katiba, kila mtu ana haki ya kuchukua hatua za kisheria, hivyo uamuzi wao ni sahihi katika kulinda demokrasia nchini.

Alisema Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) ndiyo yenye mamlaka ya kusimamia uchaguzi kwa kuzingatia sheria itakayotungwa na Bunge na walitegemea kupata sheria hizo, badala yake wameona TAMISEMI kutunga kanuni za kusimamia mchakato.

"Ibara ya 74(6) (e) inaeleza kuwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi itatekeleza majukumu yote yatakayotolewa na Bunge. Kwa mantiki hiyo TAMISEMI haina mamlaka ya kisheria kusimamia uchaguzi," alisema Wangwe.

Kaiza alisema uchaguzi uliopita ulikuwa na dosari kadhaa ikiwamo baadhi ya vyama vya kisiasa kupitisha wagombea bila kupingwa, wengine kuenguliwa na kutokuwapo uhuru na haki kwenye mchakato wa kuwapata viongozi.

Alisema wameamua kufungua shauri kupinga TAMISEMI kusimamia uchaguzi ili kuondoa dosari zilizojitokeza kwenye uchaguzi uliopita na kwamba katika uchaguzi wa mwaka huu, wanataka uwe huru, haki na wenye kuzingatia misingi ya demokrasia.



Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la Katiba Tanzania, Bob Wangwe (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, akiwataka wananchi wajitokeze katika Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Dar es Salaam kusikiliza shauri la kupinga TAMISEMI kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji. Kulia ni Mwenyekiti wa Jukwaa hilo, Dk. Ananilea Nkya na Mwanaharakati, Bubelwa Kaiza. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# PM ahimiza vyuo kuzalisha wahitimu wenye maarifa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI Mkuu Kassim Majiliwa ameitaka Taasisi ya Sayansi na Teknoloji ya Karume (KTIS) na zingine za mafunzo kuzalisha wahitimu wengi wenye maarifa na ujuzi unaohitajika katika soko la ajira.

Aliyasema hayo jana visiwani hapa wakati akizungumza katika sherehe za kuadhimisha kutimia miaka 50 tangu kuanzishwa kwa idara ya ujenzi ya Chuo cha Sayansi na Teknolojia (KIST), alipomwakilisha Rais Dk Samia Suluhu Hassan.

Alisema kufanya hivyo ni kuongeza kiwango cha kazi na ubobezi ambazo zinafanywa na wazawa na kupunguza matumizi ya wataalamu wa kigeni na ikibidi wakigeni watumike katika kujenga na kuimarisha uzoefu kwa watanzania.

Aliwataka waajiri wote kuweka utaratibu wa kuajiri wahandisi wahitimu wa ndani ili kuwajengea uwezo wakati wakiwa kazini kwa manufaa taifa.

Aidha, alitaka ushirikiano kwa taasisi zinazotoa mafunzo kutenga nafasi ya kuwapokea vijana waliopo vyuoni na serikali inaendelea kuweka mkazo kwenye elimu ya juu na kuwataka vijana wa Tanzania kuchangamkia fursa kwa mafunzo katika fani ya Sayansi na Teknolojia ambayo serikali kwa sasa imeweka kipaumbele.

Alisema uhandisi ni taaluma inayopaswa kuzingatia miiko na maadili na kwamba ni vyema wahandisi wakafuata maadili kwa miradi wanayoisimamia inakidhi viwango vya kimataifa.

Alisema bodi za wasajili zina wajibu kwa mujibu wa kisheria kusimamia maadili ya wahandisi na kampuni za kihandisi na kutekeleza wajibu wao wa kusimamia kikamilifu taaluma ya kihandisi kwa kuzingatia sheria na kanuni.

> **Alisema taasisi hiyo ina umuhimu mkubwa katika taifa hasa ikizingatiwa kuwa inatoa mafunzo ya kitaaluma ya Sayansi na Teknolojia, pia inachangia kukuza utafiti na ubunifu ...**

Aidha, alisema taasisi hiyo imesaidia kuzalisha ajira kwa kutoa wahitimu mahiri wa Sayansi na Teknolojia na ina mchango mkubwa kupunguza tatizo la ajira.

Alisema kila mmoja anatambua na kuthamini mchango unaotolewa na wasanifu, wahandisi, wakadiriaji majengo pamoja na wataalamu wengine katika kuleta maendeleo ya nchi.

Pia, wito umetolewa kwa Watanzania hasa watalaamu wa uhandisi, kuunda kampuni binafsi na zipo fursa kuunda kampuni na kuzisajili na serikali ina miradi mingi na inataka kupunguza kuagiza kampuni kutoa nje na badala yake kuzitumia za ndani.

Alisema kuna ongezeko kubwa la miundombinu ya aina mbalimbali na katika miradi yote wahandisi wametoa mchango mkubwa kuimarisha ujenzi wa miundombinu hiyo.

Aidha, serikali imekuwa ikiimarisha majengo ili kuwawezesha wasomi kusoma katika mazingira bora kwa lengo la kuwa wabobezi katika fani wanazosomea.

Alizitaka taasisi za sekta binafi kutengeneza wigo kuhakikisha chuo hicho kinapanda kwa kufungua dirisha la kuwaleta wasomi kuja kufanya kazi kwa muda mfupi.

Majaaliwa alisema kwa kutambua mchango wa wahandisi serikali ya awamu ya kwanza chini ya uongozi wa Rais Karume ilianzisha chuo cha ufundi Karume na hadi sasa kinaimarika.

Taasisi hiyo imeendelea kutoa wahitimu mahiri duniani kote na tangu kupandishwa hadhi imeshatoa wahitimu 335 wakiwamo wanawake 108.

Alisema taasisi hiyo ina umuhimu mkubwa katika taifa hasa ikizingatiwa kuwa inatoa mafunzo ya kitaaluma ya Sayansi na Teknolojia, pia inachangia kukuza utafiti na ubunifu na kusisitiza kuwa utafiti unaofanywa usiishie katika maonesho bali uingie katika masoko.

Alitoa wito kwa taasisi binafsi kutengeneza wigo ili taasisi hiyo ya KITS kupanda na kufungua milango kwa wasomi kutoka nje kuja kujifunza japo kwa muda mfupi.

Mkuu chuo, Dk. Mahmoud Abdulwahabi, alisema taasisi hiyo iliyoanzishwa mwaka 1966 ilianza kutoa mafunzo kwa fani mbili ambazo ni ufundi mitambo na umeme na ilipofika mwaka 1975 ilianza kutoa mafuno ya uhandisi ujenzi na sasa inatoa mafunzo fani 18 kwa ngazi ya shahada na stashahada.

Alisema serikali inaimarisha sekta ya afya kwa kujenga hospitali na vifaa tiba na katika kuunga mkono hilo imeazisha kozi ya injinia wa umeme na vifaa tiba.

Mwenyekiti wa Baraza wa KIST, Dk. Afua Khalfani Mohamed, alisema kwa miaka 50 ni dhahiri imeshajijengea uzoefu mkubwa na hatua kubwa imechukuliwa licha ya changamoto mbalimbali ikiwamo ya miundombinu. Alisema bado taasisi inahitaji kufundisha watalamu mbalimbali wa teknolojia na misaada ili kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia duniani na kupiga hatua.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhamed Mussa, alimpongeza Rais Samia kwa kuwa mhandisi bingwa Tanzania kwa kujenga miundombinu ya kisasa ikiwamo barabara, reli ya kisasa na usafiri wa anga.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Agizo kuhusu ukaguzi wa mara kwa mara wa magari utekelezwe

**MAADHIMISHO** ya kilele cha Wiki ya Usalama Barabarani yalifanyika juzi jijini Dodoma huku Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwa mgeni rasmi. Shughuli mbalimbali zilifanyika katika maadhimisho hayo yakiwamo maandamano ya vyombo vya moto na taarifa mbalimbali pamoja na takwimu za ajali za barabarani ambazo zimeonekana kuongezeka mwaka hadi mwaka.

Kuhusu ajali za barabarani, kwa mwaka 2023 ajali za barabarani zilikuwa 1,733 zilizosababisha vifo vya watu 1,647 wakati zilizotokana na pikipiki katika kipindi hicho zilikuwa 435 zilizosababisha vifo 332 ikilinganishwa na ajali 376 zilizosababisha vifo 332.

Kwa mujibu wa takwimu hizo, ajali za barabarani zitokanazo na magari na pikipiki, zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka na kugharimu maisha ya mamia ya Watanzania huku wengine wakiachwa na ulemavu wa kudumu.

Sababu kubwa ambazo zimekuwa zikitajwa kuwa chanzo cha tatizo hilo ni ubovu wa magari na uzembe wa madereva, pia rushwa kwa baadhi ya askari na maofisa wa usalama barabarani imekuwa ikitajwa kwamba ni chanzo kimojawapo.

Kutokana na takwimu hizo, Dk. Mpango alitoa maagizo kadhaa katika kudhibiti ajali hizo ikiwamo kufanyika kwa ukaguzi wa mara kwa mara wa magari.

Aliweka bayana kwamba mfumo wa sasa wa ukaguzi wa magari unaofanyika mara moja kila mwaka, tena wakati wa Wiki ya Nenda kwa Usalama, umepitwa na wakati. Kutokana na ukweli huo, Dk. Mpango aliagiza ukaguzi ufanyike angalau mara nne kila mwaka, kwa maana ya kila baada ya miezi mitatu.

Sambamba na Dk. Mpango aliagiza udhibiti wa magari yanayobeba wanafunzi, mengi yakiwa ya shule binafsi ambayo alisema hayana ubora unaostahili ndiyo maana yamekuwa yakisababisha ajali na wanafunzi, yakiwamo mawili mkoani Arusha ambayo yaligharimu maisha ya wanafunzi.

Pamoja na maagizo hayo yote ikiwamo matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika kudhibiti ajali za barabarani, suala la ukaguzi wa magari mara kwa mara tena kila robo mwaka ni mwafaka.

Hatua hiyo ni ya kuungwa mkono, hivyo inapaswa kutekelezwa na vyombo vinavyohusika vikiwamo Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) na jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani.

Kama wahenga wasemavyo kisu kimegonga mfupa, ukaguzi wa magari na vyombo vingine vya moto mara kwa mara, utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikidaiwa kuwa zinatokana na ubovu wa magari.


Haiingii akilini kuona vyombo vya moto ambavyo vinabeba dhamana kubwa ya maisha ya wanadamu vinafanyiwa ukaguzi mara moja kwa mwaka.

Utekelezaji wa suala hili uko wazi na wala hauhitaji kuwapo mijadala kwa mustakabali wa maisha ya Watanzania kwa kuwa utawezesha kulinda nguvu kazi ya taifa ambayo imekuwa ikiteketea kila uchao kwa ajili za magari. Katika suala hili, hakuna kuoneana haya wala huruma kwa sababu kufanya hivyo kutasababisha Watanzania waendelee kutoa machozi kwa kupoteza ndugu zao ambao huangamia kutokana na ajali za barabarani.

Ni kweli kwamba magari mengi hasa mabasi yanayosafirisha abiria ndani ya miji na kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine ni mabovu kiasi kwamba yanasababisha abiria kuwa na wasiwasi kutokana na hali yalivyo.

Ni imani kwamba iwapo ukaguzi utafanyika, kuna uwezekano mkubwa wa magari mabovu na yasiyokidhi viwango yakawekwa kando katika kutoa huduma za usafiri kwa abiria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kaulimbiu ihamasishe kujitokeza kusajiliwa

Na Sabato Kasika

**NOVEMBA** mwishoni mwaka huu, ni kuchagua viongozi wa serikali za mitaa, na baadaye 2025 ni uchaguzi mkuu wa rais, wabunge, wawakilishi na madiwani

Wakati huu ambao nchi inaelekea katika uchaguzi huo, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), nayo iko mikoani ikiendelea kuboresha daftari la kudumu la wapigakura.

INEC inafanya kazi hiyo, ikichagizwa na kaulimbiu isemayo: " Kujiandikisha kuwa mpigakura ni msingi wa uchaguzi bora", ambayo inahimiza Watanzania kutambua umuhimu wa kujiandikisha na kushiriki katika uchaguzi.

Kwa kaulimbiu hiyo, ni wazi kuwa tume imedhamiria kufanya mchakato wa uchaguzi kuwa bora zaidi, iwapo kila mwananchi mwenye sifa atashiriki tangu hatua ya kwanza hadi mwisho.

Katika mzunguko wa sasa unaoendelea wa kuboresha daftari hilo wapo waliojiandikisha kwa mara ya kwanza kwa kutimiza miaka 18, hivyo, watashiriki uchaguzi wa serikali za mitaa.

Huenda kufikia uchaguzi mkuu mwakani, wakawepo wengine watakaokuwa wametimiza miaka hiyo wakati huo.

Mchakato unaoendelea sasa ni wa muhimu, kwa kuwa ndio unaohimizwa na kaulimbiu, inayohimiza kutaka kila Mtanzania mwenye sifa ajiandiakishe ili achague viongozi wa nchi.

Hivyo, kila anayejua kwamba ana sifa za kuwa mpigakura, katika uchaguzi ujao, ajitokeze ili tume imuorodheshe katika daftari la kudumu la wapigakura au iboreshe taarifa zake.

Miongoni mwa sifa zinazotajwa na tume ambazo mtu anatakiwa kuwa nazo ni uraia wa Tanzania, umri wa miaka 18 na akili timamu,

Kwa kuwa kujiandikisha kuwa mpigakura ni msingi wa uchaguzi bora, Watanzania hawana budi kulitambua hilo na kulifanyia kazi.

Kwa nini? Kwa sababu wapo baadhi ya watu ambao husema hawaoni umuhimu wa kupiga kura, kwa maelezo kwamba hata wakimpigia mgombea wanayemtaka, anashinda mwingine wasiyemtaka.

Hiyo ni miongoni mwa sababu zao, lakini sidhani kwamba kususa ni sawa, kwani kususa kunamfanya mgombea asiyetakiwa kushinda kirahisi.

Hivyo, njia nzuri ni kuendelea kupiga kura katika mazingira yoyote badala ya kususia na kuwafanya wengine kuchagua mgombea usiyemtaka.

Ninaamini elimu ya mpigakura inaendelea kutolewa wakati huu ambao tume inaboreaha daftari la kudumu la wapigakura, hivyo, tuitumie kutambua haki za kuboresha taarifa zetu ili baadaye tushiriki katika uchaguzi.

Kitendo cha tume kuja na kaulimbiu hiyo, kinaonyesha imedhamiria kuboresha uchaguzi, hivyo, ingekuwa ni vyema kuiunga mkono kwa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha na kuboresha taarifa za kila raia.

Vilevile, tunapokwenda kuboresha taarifa zetu au kujiandikisha, ni muhimu kuepuka mambo kadhaa ambayo tume inayataja, ikiwamo mtu kutoa taarifa zake lakini za uongo.

INEC pia inasema ni makosa kutoa taarifa za uongo za mtu mwingine kwa lengo la kuandikishwa kuwa mpigakura, hivyo, hairuhusu hilo litokee.

Pia, wananchi wanatakiwa kuepuka kuomba kuandikishwa zaidi ya mara moja au kutoa tamko la uongo kuhusu kupotea au kuharibika kwa kadi ya mpigakura ama kifo.

Mwananchi pia anatakiwa kuepuka kununua au kuuza kadi ya mpigakura na kuiba ama kuharibu kadi ya mpigakura, mkazo ukiwa ni kaulimbiu ya "kujiandikisha kuwa mpigakura ni msingi wa uchaguzi bora".

Ninaamini hayo yakizingatiwa, lengo la tume la kuandikisha wapigakura wapya 5,586,433 litatimia, lakini pia lengo la kuboresha taarifa za wapigakura litawezesha kupata vijana na raia wengi zaidi kushiriki zoezi hilo la kidemokrasia.

Kumbuka uchaguzi wa viongozi wa mchakato wa kidemokrasia ambao unampa kila raia nafasi ya kumchagua anayeamini anafaa kumuongoza.

## HABARI KITAIFA

# Nsekela, viongozi wa dini wateta katika uzinduzi Akaunti ya Sadaka

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela amekutana na viongozi wa dini katika hafla ya uzinduzi wa Akaunti ya Sadaka, mahsusi kwa ajili ya taasisi za dini kukusanya sadaka, zaka na michango mingine inayolenga kurahisishia waumini kumtolea Mwenyezi Mungu wakati wa ibada au hata wanaposhindwa kuhudhuria ibada.

Katika hafla hiyo, mamia ya viongozi na waumini wa dini na madhehebu mbalimbali nchini wamepongeza ubunifu uliofanywa na benki hiyo kwa kuja na Akaunti ya Sadaka ambayo itaongeza ukaribu kati ya waumini na nyumba zao za ibada.

Akizungumza kuhusu Akaunti ya Sadaka, Naibu Katibu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padre Chesco Msaga alisema ni mapinduzi yatakayosaidia kukumbusha Wakristo kumtolea muumba wao ili kukamilisha kazi kubwa ya uenezi wa injili nchini na duniani kwa ujumla.

"Maisha ya mwanadamu hayana maana yoyote hapa duniani asipomwabudu muumba wake na kumtolea zaka na sadaka kama ilivyoagizwa katika Biblia Takatifu.

"Ninawapongeza Benki ya CRDB kwa ubunifu huu na ninawaomba wakristo kote nchini kuiona fursa hii ya kumtolea Bwana kirahisi," alisema Padre Msaga.

Naibu Katibu huyo wa TEC alisema fursa zinazoletwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia zinapaswa kutumiwa na wakristu kuimarisha ukaribu wao na Mwenyezi Mungu na kumtolea sadaka na zaka pamoja na michango mingine ni kati ya njia kuu za kutimiza agano na kuieneza injili takatifu.

Akizungumza kwa niaba ya Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Dk. Abubakary Zubery Bin Ally, Sheikh Hilal Shaweji, almaarufu Sheikh Kipozeo, naye alipongeza ubunifu uliofanywa akisema utawafaa sana Waislamu kushiriki kutoa sadaka ambayo ni kati ya nguzo muhimu za dini ya Kiislamu. "Waislamu tumeagizwa kutoa sadaka na zaka. Tumeagizwa kutoa sadaka kwa ajili ya kuwasaidia wasiojiweza na kuendeleza Uislamu duniani.

"Ubunifu uliofanywa na Benki ya CRDB unaturahisishia kutimiza msingi huu muhimu kwa imani yetu. Tusiwe tena na sababu ya kuwa mbali na Mwenyezi Mungu," alisema Sheikh Kipozeo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela alisema kuwa siku zote wamekuwa wakijitahidi kubuni huduma na bidhaa zinazokidhi mahitaji na matarajio ya wateja ukigusa sekta tofauti ukiwamo utamaduni na imani za watu watu wanaowahudumia.

"Maneno matakatifu yanasema binadamu aliumbwa ili amtukuze muumba wake. Hili ni jukumu letu wanadamu kwa kipindi chote cha maisha yetu hapa duniani.

"Katika kumtukuza Mwenyezi Mungu, tunakumbushwa kumtolea sadaka na zaka pia. Azma ya Benki yetu ya CRDB siku zote imekuwa kukidhi matarajio na mahitaji ya wateja wetu na jamii tunayoihudumia kwa ujumla.

"Katika kufanikisha hili tumekuwa tukibuni huduma na akaunti zinazoendana na misingi ya imani pamoja na maeneo mengine, mfano biashara, uwekezaji na utunzaji akiba," alisema Nsekela.

Katika jitihada hizi, Nsekela alisema tayari Benki ya CRDB imebuni Huduma za Al Barakah zinazoendana na imani ya Kiislamu, lakini kuna fursa ya kuwahudumia zaidi waumini wote pamoja na taasisi za dini kwa ujumla ndio maana sasa imeleta Akaunti ya Sadaka.

Mkurugenzi alihimiza Watanzania kumtolea Mwenyezi Mungu fungu lake bila kukosa kwa kuwa benki hiyo imeondoa ugumu uliokuwapo mwanzoni.




Mufti wa Tanzania, Dk. Zubery bin Ally (kulia) akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa pili kulia), katika uzinduzi wa Akaunti ya Sadaka, jijini Dar es Salaam. Wengine (kutoka kushoto) ni Naibu Katibu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padre Chesco Msaga, Rais wa Manabii na Mitume, Nabii Joshua Aram Mantyala, Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Azania Front, Mchungaji Charles Mzinga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mashirika 40 tegemezi kupigwa panga

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SERIKALI kwa mwaka wa fedha 2024/25, inatarajia kufuta taasisi na mashirika ya umma 40 yaliyoshindwa kujiendesha kwa kutegemea ruzuku na gharama za uendeshaji kutoka serikali kuu.

Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelekea ufunguzi wa kikao kazi cha wenyeviti wa bodi na watendaji wakuu wa taasisi za umma.

Kwa mujibu wa Mchechu, mkutano huo utafunguliwa leo na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na unatarajiwa kufanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC).

"Tutakuwa na taasisi ambazo tunaona mchango wake,ndani ya pato la serikali ambazo pia tunaziona zikipunguza utegemezi kutoka katika mfuko wa serikali.

"Tunafikiri mwaka huu tunapoenda kuumaliza na kuanza mwaka ujao wa fedha, lengo letu ni kupunguza taasisi tegemezi kwa serikali ikiwamo kulipiwa mishahara na serikali au gharama za uendeshaji angalau taasisi 30 mpaka 40," alisema.

Mchechu alisema wakifanikiwa kwenye jambo hilo, watawaeleza wanaochangia mfuko huo kuongeza kasi ya kuchangia gawio na serikali itakuwa na fedha za kutosha za kutoa huduma muhimu za kijamii.

**"Tunafikiri mwaka huu tunapoenda kuumaliza na kuanza mwaka ujao wa fedha, lengo letu ni kupunguza taasisi tegemezi kwa serikali ikiwamo kulipiwa mishahara na serikali au gharama za uendeshaji angalau taasisi 30 mpaka 40,"**

Pia alisema Ofisi ya Msaili wa Hazina imepewa jukumu la kusimamia uwekezaji wa umma mahali popote ikiwamo kwenye mashirika ya umma na nje ya mashirika hayo.

Alisema kwa sasa wana mashirika ya umma 248 na yasiyokuwa ya umma 58 ambayo serikali ina gawio la kuanzia asilimia 50 kushuka chini.

Mchechu pia alisema uwekezaji wa mashirika hayo una thamani ya Sh. trilioni 76 na kuelekea kufunga hesabu za mwaka huu, wanatarajia uwekezaji utaongezeka kutokana na utendaji kazi unaoendelea kufanywa na serikali.

"Hizi Sh. trilioni 76 ni fedha nyingi sana katika hatima ya Watanzania kwa kuwa ni uwekezaji mkubwa kupitia serikali na ni kitu muhimu kwa uchumi wetu," alisema Mchechu.

Alisema kundi la washiriki wa mkutano huo wanaokutana mkoani humo, ndio wanasimamia mapato yasiyokuwa ya kikodi kwa zaidi ya asilimia 95 kwa mapato hayo serikali inapata kwa sehemu kubwa kupitia uwekezaji wake.

"Kikao hiki ni muhimu sana kwa kuwa kwa sehemu kibwa kinagusa uchumi wa nchi na wamefanikiwa kufanya mabadiliko mengi na maboresho ya usimamizi wa taasisi hizi," aliongeza.

Mchechu pia alisema taasisi zilizochangia mwaka wa fedha uliopita kutoa gawiwo kwa serikali ziliongezeka kutoka taasisi 109 mpaka 145 na ongezeko ni taasisi 36.

Alisema katika kipindi cha mwaka huu wa fedha wameimarisha mafunzo ya bodi zinazoongoza hizo taasisi,kutoa miongozo mbalimbali ikiwamo uimarishaji wakazi.

Kadhalika, alisema katika kikao hicho, watakuwa na mawasilisho mbalimbali yatakayofanywa na watoa mada wa ndani ya nchi na nje na kikao kimejikita kuzisukuma taasisi za umma kuanza kufikiria uwekezaji nje ya mipaka ya Tanzania.

Mchechu alisema washiriki watapata fursa ya kubadilishana uzoefu kupitia maazimio waliyokubaliana katika kikao cha mwaka jana, kukumbushana matarajio ya serikali na kuweka mipango mkakati ya mwaka huu.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara (katikati waliokaa), akiwa katika picha ya pamoja na wadau waliohudhuria Mkutano wa 27 wa Kamati ya Kusimamia Utekelezaji wa Hati ya Makubaliano ya Ukaguzi wa Meli katika Bahari ya Hindi (IOMOU), jijini Dar es Salaam jana, wenye lengo la kujadili na kubadilishana uzoefu juu ya ukaguzi meli zinazoingia katika bandari za nchi wanachama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Daraja la Nyerere kukabidhiwa baada ya bil. 344/- kupatikana

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

MRADI wa Daraja la Nyerere Kigamboni ulioko wilayani Kigamboni, mkoani Dar es Salaam, unatarajiwa kukabidhiwa serikalini baada ya kukusanywa Sh. bilioni 344, ambazo ni gharama za uwekezaji uliofanywa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, aliyasema hayo jana bungeni wakati anajibu swali la Mbunge wa Kigamboni, Faustine Ndungulile (CCM).

Mbunge huyo alitaka kujua lini NSSF itakamilisha makusanyo ya deni la ujenzi wa Daraja la Nyerere Kigamboni na kulikabidhi daraja hilo serikalini.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema mfuko wa NSSF ulianza rasmi uendeshaji Daraja la Nyerere mwezi Mei 2016.

Alisema hadi kufikia mwezi Julai mwaka huu, jumla ya Sh. bilioni 102.18 zimekusanywa kutokana na tozo mbalimbali.

"Kwa mujibu wa taarifa ya upembuzi yakinifu wa mradi wakati wa kuanzishwa kwake, mradi utarejesha fedha za mfuko kiasi cha Sh. bilioni 344 hadi kukamilika kwake kwa kipindi cha miaka 30," alisema.

Katambi alisema fedha hizo ni gharama za uwekezaji pamoja na ulinzi na thamani ya fedha iliyowekezwa na kwamba, baada ya kurejeshwa mradi utakabidhiwa serikalini.

MEDIA COUNCIL OF TANZANIA

**NOTICE FOR CONVENING OF THE 26TH NATIONAL GENERAL CONVENTION**

The Vice President of the Media Council of Tanzania (MCT) hereby notifies MCT members, in accordance with Article 13 of the MCT Constitution, that the 26th National General Convention (NGC) of the Media Council of Tanzania (MCT) will be held in Dar es Salaam on Friday, September 27, 2024. The Venue and time of the meeting will be determined in due course.

The proposed agenda at the 26th NGC is as follows:

1. Opening;
2. Adoption of Agenda;
3. Introduction & Remarks of newly appointed MCT Executive Secretary;
4. Confirming Minutes of the 25th National General Convention held at the African Court of People and Human Rights conference, in Arusha on September 28, 2023;
5. Matters arising from the 25th NGC;
6. Report of the Executive Secretary;
7. Adoption of 2023 Audited Financial Statements;
8. Appointment of External Auditor for the period ending December 31, 2024;
9. Election of MCT President/ Ratification of appointment of MCT President;
10. A.O.B;
11. Closing.

MCT members who have not paid their annual subscription fees by the deadline are reminded to do so immediately.

*Yussuf Khamis Yussuf*

Vice President
Media Council of Tanzania (MCT)

# 'Usafiri majini utachochea ukuaji uchumi wa Tanzania'

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara amesema serikali inatekeleza mipango madhubuti ya kuchochea ukuaji uchumi wa Tanzania kwa kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya usafiri wa majini.

Prof. Kahyarara aliyasema juzi wakati akifungua Mkutano wa 27 wa Kamati ya Kusimamia Utekelezaji wa Hati ya Makubaliano ya Ukaguzi wa Meli katika Bahari ya Hindi (IOMOU), wenye lengo la kujadili na kubadilishana uzoefu kuhusu ukaguzi wa meli zinazoingia katika bandari za nchi wanachama.

Alisema serikali imewekeza katika bandari, hali inayochochea mageuzi makubwa na kuleta matunda yenye tija kubwa, ikiwamo kupunguza foleni za meli kusubiri kutia nanga kutoka meli 40 hadi kufikia meli 18 kwa siku.

"Kwetu Tanzania, Bahari ya Hindi ni muhimu kwa sababu, asilimia 98 ya biashara za nje zinapita katika Bahari ya Hindi," alisema Prof. Kahyarara.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Mohamed Salum alisema TASAC imefarijika kupata fursa ya kuratibu na kuandaa mkutano huo wa kimataifa kwa nchi za ukanda wa Bahari ya Hindi.

Alisema mkutano huo unatoa fursa kwa nchi wanachama kubadilishana uzoefu kuhusu ukaguzi wa meli zinazoingia katika bandari za nchi wanachama.

"Wataalamu kutoka maeneo mbalimbali duniani wamekutana kuanzia leo (juzi) Agosti 26-30 mwaka huu, ili kujengeana uwezo wa namna bora ya kushirikiana katika kutekeleza makubaliano ya ukaguzi wa meli za kimataifa zinazoingia bandarini," alisema.

Salum alisema waday hao pia wanajadiliana namna ya kuimarisha udhibiti wa usalama, ulinzi wa vyombo vya usafiri na utunzaji mazingira majini.

Mkutano huo wa 27 wa IOMOU unafanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Nchi 14 zinashiriki ambazo ni Australia, Afrika Kusini, Comoro, Kenya, Msumbiji, Madagasca, Msumbiji, Visiwa vya Shelisheli, India, Iran, Japan, Myamar, Sri Lanka na wenyeji Tanzania.

IOMOU inaadhimisha miaka 25 tangu kuanzisha makubaliano hayo na Tanzania ikiwa ni miongoni mwa nchi sita za mwanzo kukubali kutia saini mkataba huo ambao kwa sasa kuna nchi zaidi ya 20 zinazoshirikiana katika kuutekeleza.

IOMOU inalenga kubaini na kukomeza meli zilizo chini ya kiwango katika Bahari ya Hindi.

HABARI KITAIFA

# Marufuku viongozi, mawakala kuingilia uandikishaji wapigakura

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), imepiga marufuku viongozi na mawakala wa vyama vya siasa kuingilia mchakato wa uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura kwa wananchi unaotarajiwa kuanza kufanyika mkoani hapa Septemba 4 hadi Septemba 10 mwaka huu.

Amri hiyo ilitolewa jana na Mjumbe wa Tume hiyo, Jaji Asina Omari wakati wa mafunzo kwa watendaji ngazi ya mkoa huo kuhusu uboreshaji wa daftari hilo.

Jaji Asina, alisema ni muhimu kwa mawakala hao kuwepo kwenye vituo hivyo kwa kuwa watasaidia kuleta uwazi, kuwatambua waombaji wa eneo husika na kuondoa vurugu zisizokuwa za lazima.

Alisema maelekezo yatatolewa na wakufunzi vituoni ni muhimu kufuatwa na mawakala, viongozi wa vyama hivyo na wananchi watakaofika kuandikishwa.

Jaji Asia, alisema INEC imetoa kibali cha kutoa elimu ya mpigakura kwa asasi za kiraia 157 na 33 kwa zile za uangalizi na vitambulisho ili watambulike.

**Jaji Asia, alisema INEC imetoa kibali cha kutoa elimu ya mpigakura kwa asasi za kiraia 157 na 33 kwa zile za uangalizi na vitambulisho ili watambulike.**

Aliwaomba kutunza vifaa vinavyotumika kufanya kazi kwa kuwa vimenunuliwa kwa bei kubwa na vinatakiwa kwenda kutumika maeneo mengine nchini. Mkaguzi wa Uhamiaji Mkoa wa Manyara, Castor Makungu, akitoa mada kuhusu kumtambua raia halali, alisema maofisa uandikishaji wanatakiwa kuwa makini kuwatambua raia wa Tanzania watakaofika vituoni na wakimtilia mtu shaka ni vizuri kuwashirikisha maofisa wa idara hiyo wa wilaya.

Makungu, alisema iwapo watamtilia mtu shaka kuhusiana na uraia wake, ni vema wakasubiri hadi Ofisa uhamiaji atakapofika kumhoji na kujiridhisha.

Kaimu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Manyara, Gerald Chembe aliipongeza INEC kwa kuruhusu wafungwa kujiandikisha kupiga kura, akisema ni jambo jema.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Fakii Lulandala (katikati), akizungumza kwenye kikao kuhusu uvunaji misitu, kupunguza kero na migogoro inayotokana na ardhi, ofisini kwake Orkesumet, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mwalimu akutwa chumbani amekufa

**Na Steven William,** MUHEZA

MWALIMU wa Shule ya Msingi Kwelubuye iliyopo Kata ya Kicheba wilayani hapa Mkoa wa Tanga, Deogratius Masawe, amekutwa amekufa chumbani kwake katika nyumba aliyokuwa anaishi eneo la National.

Akizungumza na NIPASHE jana, Katibu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) wa Wilaya ya Muheza, Seleman Mashaka, alisema kifo cha Masawe kimegundulika baada ya rafiki zake kwenda nyumbani kwake.

Mashaka, alisema rafiki zake hao walichukua uamuzi huo baada ya mwenzao huo kutoonekana mitaani tangu Ijumaa iliyopita. "Baada ya siku hiyo hakuonekana tena, mpaka rafiki zake walipomtafuta nyumbani kwake na kukuta amefariki," alisema.

Alisema baada ya kufungua mlango wa chumba hicho, walikuta mwili wa mwalimu huyo ukiwa umeanza kuharibika.

Kwa upande wake jirani wa mwalimu huyo Fikirini Masokola, alisema kuwa ijumaa iliyopita alionana na mwalimu huyo nyumbani kwake akiwa na pikipiki yake.

Alisema walisalimiana na baadaye kila mmoja akaendelea na shughuli zake.

Masokola, alisema juzi walifika rafiki zake nyumbani hapo kumfuata kwa kuwa walikuwa hawamuoni na simu yake ilikuwa haipatikani.

Alisema walipomuuliza alipo mwalimu huyo aliwajibu hajaonana naye kwa kipindi cha siku tatu na kuwashauri wachungulie ndani kama amelala.

Alisema walichungulia ndani kupitia dirishani, walimuona amelala kitandani na kubaini alikuwa amekwisha kufa na kutoa taarifa polisi.

Asakri wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Muheza, wakiongozwa na Mkaguzi. Leonard Bandola na Diwani wa Kata ya Genge, Mosses Kisiki walifika nyumbani kwa mwalimu huyo na kuvunja mlango na kukuta mwili wake ukiwa umeanza kuharibika. Baada ya kufanya uchunguzi wa awali, mwili huo ulipelekwa kuhifadhiwa chumba cha maiti cha Hospital ya Wilaya Muheza na kusafirishwa kwao mkoani Kilimanjaro kwa mazishi.

Mkuu wa Polisi Wilaya ya Muheza, Hadija Sokolo amethibitisha kutokea kwa kifo hicho na kusema wanasubiri taarifa ya kifo hicho kutoka kwa madaktari baada ya kuufanyia uchunguzi mwili wake ili kujua chanzo chake.

# Wachimbaji Tanzanite wapewa somo

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WACHIMBAJI wa Madini ya Tanzanite katika mji mdogo wa Mirerani Wilaya ya Simanjiro mkoani hapa, wametakiwa kuchimba kwa usalama kwa kupambana na vumbi na moshi wa baruti ili kuepuka magonjwa ya vifua.

Ofisa Madini Mkazi Mirerani, Nchagwa Marwa alitoa kauli hiyo wakati wa uchaguzi wa kamati za usuluhishi na usalama migodini kitalu B na D katika machimbo ya madini hayo.

Marwa, alisema wamiliki wa migodi wanapaswa kuhakikisha maji yanakuwepo kwa ajili ya kuondoa vumbi migodini na kupuliza hewa ya kutosha ili kuondoa moshi wa baruti.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (MAREMA), Justin Nyari, aliwapongeza viongozi waliochaguliwa na kuwataka wasimamie haki bila upendeleo.

Katibu wa MAREMA Tawi la Mirerani, Rachel Njau, alisema baada ya uchaguzi wa kamati hizo, kitachofuata ni uchaguzi wa viongozi wa chama hicho Tawi la Mirerani.

# Wazazi waonywa kwa kurubuni watoto wafeli mitihani

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Monduli, Festo Kiswaga amewaonya wazazi wenye tabia ya kuwarubuni wanafunzi kufanya vibaya katika mitihani ya darasa la saba ili wakachunge mifugo na kuwaoza.

Kiswaga alitoa onyo hilo jana wakati akizungumza na wazazi katika Shule ya Msingi Mswakini.

"Tangu nije wilaya hii ya wafugaji nimegundua kuna tabia ya watu kushawishi watoto wao na baadhi kuwatisha ili wafeli mitihani yao na kuwapeleka machungani na watoto wa kike wawaoze, acheni tabia hii," alisema

Mkuu huyo wa wilaya, alisisitiza kuwa serikali haiwatafumbia macho wazazi wa aina hiyo na kwamba itafuatilia kila eneo ili kuhakikisha kila mtoto atakaye-





# Baba jela kwa kumpa ujauzito bintiye

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita mkoani hapa, imemhukumu Shija Lucas (40), mkazi wa Kijiji cha Nyarubele-Kasamwa kifungo cha miaka 30 jela kwa kumnajisi bintiye (14) na kumpa ujauzito.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Joseph Daudi baada ya ushahidi uliotolewa mahakamani hapo kuthibitisha pasipo kuacha shaka kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Hakimu Daudi, alisema mahakama hiyo imetoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa akina baba wengine wenye tabia kama yake ya kuwanajisi watoto wao.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Godfrey Odupoy, ulipeleka mashahidi wanne mahakamani hapo na vielelezo viwili ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo, alitenda kosa hilo.

Alisema siku tofauti katika Kijiji cha Nyarubele-Kasamwa, mshtakiwa huyo alikuwa akimnajisi binti yake huyo ambaye alikuwa akiishi naye nyumbani kwake wakati mkewe anapokuwa amesafiri na kumpatia ujauzito.

Alisema binti huyo alipelekwa Kituo cha Polisi Kasamwa na kupewa PF3 kisha Kituo cha Afya Kasamwa, ambako daktari alifanyia uchunguzi na majibu ya vipimo kuthibitisha kuwa amenajisiwa na kupata ujauzito wa miezi mitatu.

> **Alisema siku tofauti katika Kijiji cha Nyarubele-Kasamwa, mshtakiwa huyo alikuwa akimnajisi binti yake huyo ambaye alikuwa akiishi naye nyumbani kwake wakati mkewe anapokuwa**

Alipompatia fursa ya kujitetea, mshtakiwa huyo aliiomba mahakama hiyo impunguzie adhabu kwa madai kuwa ana familia na wazazi wake wanamtegemea na pia ni kosa lake la kwanza.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili Odupoy uliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo kwa mujibu wa sheria.

Akijibu maombi ya mshtakiwa huyo, Hakimu Daudi alitupilia mbali utetezi wake na kukubaliana na upande wa mashtaka kwa kumhukumu kifungo hicho jela.

"Kosa hili ulilolshtakiwa nalo adhabu yake haina mbadala. Hivyo mahakama hii inakuhukumu kutumikia kifungo cha miaka 30 jela ili ukajifunze namna ya kuishi na familia yako na ukimaliza kifungo chako utakuwa raia mwema kwa familia yako pamoja na jamii nzima. Haki ya kukata rufaa ipo wazi."

Awali akisoma hati ya mashtaka, Wakili Odupoy kati ya Febuari na Machi mwaka 2023 katika Kijiji cha Nyarubele -Kasamwa Mkoa wa Geita, mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.



Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (kushoto), akifungua mafunzo ya siku sita kuhusu mifumo ya kiteknolojia ya hali ya hewa kwa mataifa 13 kutoka barani Afrika chini ya usimamizi wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), jijini Mwanza juzi. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Ubakaji, ulawiti wakithiri shuleni Sabasaba

**Na Timothy Itembe,** MARA

JESHI la Polisi mkoani hapa, limeomba kudhibiti kukithiri kwa matukio ya ubakaji na ulawiti katika shule za msingi Sabasaba, Mapinduzi na Azimio ili kuwawezesha wanafunzi kusoma katika mazingira rafiki.

Ombi hilo la Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Sabasaba Wilaya ya Tarime mkoani hapa, Yugen Keraryo juzi katika kikao cha Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) wa kata hiyo cha kujadili maendeleo yao.

Keraryo, alisema umoja huo ulitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika shule hizo zilizopo katika kata hiyo na kubaini kero mbalimbali ikiwemo utoro wa wanafunzi, vibaka kuingia na kuharibu mali za shule.

Vilevile alisema walibaini kuwepo kwa vitendo vya wanafunzi kulawitiana shuleni na kuomba jamii kuungana kutafuta ufumbuzi wa janga hilo kwa wanafunzi.

Alikemea tabia ya baadhi ya viongozi katika kata hiyo kukumbatia na kuwafumbia macho wahalifu wa vitendo hivyo.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkaguzi Kata wa Polisi, Raphael Lyimo alithibitisha kuwepo kwa vitendo hivyo na jeshi hilo kuchukua hatua kwa kuwakamata baadhi ya wanafunzi kwa utovu wa nidhamu na kufikisha mahakamani.

Mwenyekiti Mtaa wa Chomete, John Peter, alisema wameimarisha ulinzi katika mitaa ili kukabiliana na vitendo hivyo na kuhakikisha usalama wa raia na mali zao.

Aliitaja mitaa iliyokothiri kwa uhalifu kuwa ni Sabasaba, Songambele A na B, Iganana.

# Mamlaka za hali ya hewa Afrika zatakiwa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAZIRI wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa amezitaka mamlaka za hali ya hewa Afrika kushirikiana kutoa taarifa za hali ya hewa ili kuwasaidia wananchi barani humo kukabiliana na majanga.

Prof. Mbarawa alitoa rai hiyo juzi jijini hapa wakati akifungua mafunzo ya siku sita kwa mataifa 13 kutoka Afrika yanayoendeshwa na Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO).

Alisema tahadhari kutoka mamlaka hizo zinategemewa na wananchi kwa shughuli za uvuvi na kilimo, ambao wanahitaji kujua wanapoamka asubuhi kutakuwa na hali gani ya hewa kuwaruhusu kwenda kwenye shughuli zao.

"Ninayo imani kupitia mafunzo haya washiriki wataimarika kwenye utumiaji wa teknolojia na utoaji wa taarifa sahihi za hali ya hewa, hii itasaidia kuinua uchumi wa nchi na kuiepusha jamii na majanga kama ya kimbunga kwenye maziwa na bahari kwa wavuvi," alisema Prof. Mbarawa.

Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Balandya Elikana, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuboresha huduma kwenye mamlaka zao hususani utabiri wa hali ya hewa.

Vilevile Elikana, aliwataka kubadilishana uzoefu wa namna bora ya kuendesha mamlaka hizo kuwahudumia wakulima, wavuvi na wafugaji ambao wanategemea zaidi taarifa za hali ya hewa kwenye shughuli zao za uchumi.

# Taasisi zaamriwa kulipa ushuru

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza imezionya taasisi na kampuni zitakazokaidi amri ya kulipa ushuru kwa kipindi cha siku saba zitachukuliwa hatua kwa kukwamisha ukusanyaji mapato.

Onyo hilo lilitolewa juzi katika kikao cha baraza la madiwani robo ya nne kwa mameneja wa taasisi na kampuni hizo ambazo zimekaidi kulipa ushuru kwa halmashauri hiyo na kukwamisha kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato.

Kabla ya kutoa onyo hilo, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Yanga Makaga, aliunda kamati ya watu saba kufuatilia wa taasisi na kampuni hizo.

Makaga, aliwataja wadaiwa hao kuwa ni pamoja na Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini (TARURA), Mamlaka ya Maji Mjini Sengerema (SEUWASA), Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Mgodi wa Nyanzanga.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Binuru Shekidele, alisema ameiandikia barua kampuni na taasisi hizo kuzikumbusha kulipa ushuru, lakini hadi sasa zimeshindwa kutekeleza takwa hilo la kisheria.

Mbunge wa Sengerema, Khamis Tabasamu, aliishauri halmashauri hiyo kuzingatia utozaji kodi na tozo kwa kwa taasisi na kampuni wanazoingia nazo mikataba wakati wa kusaini ili kudhibiti ukwepaji huo.

Ukurasa 12




Ukurasa 14




siasa

JUMATANO AGOSTI 28, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

# MITANDAO YA KIJAMII ILIVYO TISHIO KUFIKIA 50/50

**Na Gaudensia Mngumi**

WAKATI taifa linaelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa Novemba mwaka huu na ule mkuu wa mwakani, watetezi wa haki za wanawake wanahimiza washiriki ili kufikia uwakilishi wa ulinganifu au 50/50.

Ni kwenye uongozi wa kisiasa kuanzia viongozi wa vitongoji, mitaani na vijiji, kisha udiwani, ubunge na uwakilishi Bara na Visiwani.

Wakati wadau na taasisi mbalimbali zikihamasisha, wanawake wanazungumzia jinsi matumizi ya teknolojia ya mawasiliano kwenye mitandao ya kijamii yanavyoweza kuwarudisha nyuma kisiasa.

Ndicho chanzo cha unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake wanasiasa watiania ya kujiingiza kwenye siasa.

Taarifa ya Umoja wa Mataifa, inayozungumzia unyanyasaji wanawake kidijitali inasema unafanyika kwa njia nyingi, mfano kutangaza mambo ya ngono mitandaoni.

Unyanyasaji unatumia picha, video na sauti, japo ni za uongo na udanganyifu lakini UN inasema ni vitisho vinavyosababisha wanawake kujiweka pembeni na kuogopa kujiingiza kwenye siasa.

Njia nyingine zinazotumika ni kuweka picha, kuchapisha habari za kibinafsi au za ndani au faragha, yote hayo yakitishia hatima ya wanawake kwenye siasa.

Katika mazungumzo na Nipashe, Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), Magdalena Sakaya, anathibitisha kuwa, mitandao inatumiwa kudhalilisha wanawake na kuwachafua, na kwamba jambo hilo lilitokea kwake.

Anasema ameshitakiwa kwa familia yake kuwa ana uhusiano usio wa kimaadili na baadhi ya viongozi kwenye chama ndiyo maana amezawadiwa cheo cha Naibu Katibu Mkuu.

Anaeleza kuwa, wabaya wake walitumia video kueleza kuwa ana mienendo inayokiuka maadili na kuipeleka kwa familia yake jambo ambalo licha ya kuwa ni la kuzushwa linaondoa heshima na hata kusambaratisha familia.

Anafafanua kuwa, mitandao ya kijamii kama whatsApp, instagram, X au twiter, Tiktok zinaweza kutumika kuchafua wanawake na wale wasiokuwa na moyo mgumu si rahisi kuendelea na siasa.

Magdalena anaeleza kuwa ni kitisho kingine cha kuwanyima wanawake fursa ya kushiriki kwenye michakato ya kidemokrasia na kuongeza usawa wa kijinsia.

"Mwenendo huu unatishia uwapo wa uwakilishi wa 50/50, "anaonya mwanasiasa huyo anayetetea usawa wa kijinsia, haki na uwakilishi unaojali maslahi ya umma.

Anasema baadhi ya wanasiasa wanaweza kuzungumzia habari za kumchafua mgombea jukwaani na taarifa zikarekodiwa na kurushwa kwenye mitandaoni.

Ni mambo yanayofanyika na kwamba kunahitajika sheria za kuwabana wahusika kuanzia, mgombea anayechafua wenzake na timu yake.

Aidha, anaungwa mkono na Sophia Mwakagenda, anayeeleza kuwa, wakati akigombea ubunge kwa tiketi ya CHADEMA kwenye jimbo la Rungwe, madai kuwa ana titi moja ambapo alitangazwa na kusambazwa kwenye mitandao.

Mambo hayo yanayolenga kumchafua na kuonesha kuwa hafai kwenye ubunge hayakumkatisha tamaa na hata sasa anaendelea na ni mwanasiasa ngangari.

Sophia anawataka wanawake wanasiasa na watiania kuachana na mambo ambayo yanawaweka kwenye hatari ya kuwa sehemu ya kunyanyaswa kijinsia kwenye mitandao.



Sophia Mwakagenda.

Anatoa, mfano 'kuposti' picha ukiwa sehemu za starehe na familia yako, umevaa mavazi yasiyo na heshima na kuandika mambo yanayokera.

"Lakini tunapokwenda kuwatembelea wapigakura wetu vijijini tubadilike. Haipendezi kuvaa mavazi ya gharama kubwa na kujipamba na vito vya thamani kubwa yanayoshangaza au kukera wengine,"anasema mwanasiasa huyo aliyekuwa mbunge wa Rungwe mwaka 2015 hadi 2020.

Anawakumbusha kuwa, picha na video zao zinaweza kutumiwa kama udhaifu na zikazunguka kwenye mitandao ya kijamii kuwaangusha.

**SHERIA**

Licha ya kuwapo kwa sheria mfano ile ya Makosa ya Mtandaoni na Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, zinaonekana haziwezi kuwabana moja kwa moja watuhumiwa wanaotuma picha, video na taarifa za kunyanyasa wanawake kwenye mitandao ya kijamii.

Kwa mfano, mbunge wa viti maalumu, Felister Njau, anasema sheria ya makosa ya mtandaoni inaweza kuibua jinai na watu wakashitakiwa lakini kwenye siasa kunahitajika juhudi zaidi.

Mfano kugombea ubunge au udiwani, muda wa kuendesha kesi unaweza kuwa mrefu na uchaguzi ukamalizika bila mtuhumiwa kuchukuliwa hatua pengine baada ya kukosekana ushahidi usiotia shaka.

Anasema aliyechafuliwa anarudishwa nyuma kwa kutukanwa na kukashifiwa mitandaoni na mpinzani wake, lakini aliyemchafua akaweza kuendelea na uchaguzi akishinda akawa mbunge na bado hukumu ikiwa haijatolewa.

Anaeleza kuwa, licha ya kwamba kuna kanuni za uchaguzi zinazokataza kampeni za lugha za kuchafuana na mambo yasiyo na maadili, haitoshi ni lazima kuwa na sheria kamili inayoharamisha unyanyasaji wa wanawake kwenye mitandao ya kijamii na kuweka adhabu zake.

Felister anasema sheria iwe wazi kuwa anayenyanyasa wanawake mitandaoni afungiwe kushiriki shughuli za kisiasa kwenye uchaguzi huo na hatua zaidi dhidi yake zichukuliwe mara moja ili kulinda wanawake na uchafuzi mitandaoni.

Anasema athari za kuchafuana wanawake mitandaoni zinakwamisha uwapo na kufikia agenda ya 50/50, kadhalika kupunguza idadi ya wanawake bungeni na kwenye michakato mingine ya kisiasa hasa inayohusisha maamuzi.

**UNYANYASAJI AFRIKA**

Nchini Kenya mgombea urais na mwanasiasa mkongwe Charity Ngillu, aliyekuwa mgombea mwenza wa urais na Raila Odinga mwaka jana, amekuwa akilengwa na unyanyasaji mitandaoni, akidaiwa kuwa hajaolewa. Ni madai yanayoonesha kuolewa ni muhimu ili mtu awe mwanasiasa wakati pengi si hitaji la lazima.

Aidha, binti wa kiongozi wa upinzani Kenya, Raila Odinga naye amekuwa akinyanyaswa na mitandao ya kijamii kuwa, anashiriki uhusiano ambao haukubaliki na jamii na kwamba yote hayo ni mfano wa namna ambavyo mitandao inatumiwa kuwarudisha nyuma wanawake kwenye siasa Afrika.

Inawachafua kijamii, familia na kuondoa imani na heshima kwa wanaowaheshimu au kuwathamini.

Wanawake wanahitaji mitandao ya kijamii kujitangaza na kufikia wapigakura wakionesha kazi wanazofanya bungeni, kwenye jamii na pia kujitambulisha kwa wapigakura wasiowafahamu majimboni .

# Migomo na maandamano sasa mahakama kuwajibisha vigogo



Kiongozi wa mpito wa Bangladesh mshindi wa Tuzo ya Nobel Muhammad Yunus. **PICHA: MTANDAO**

**Na Maulid Mmbaga**

MIGOMO na maandamano yanatumiwa na wananchi kama mahakama isiyo rasmi kuwawajibisha viongozi katika mataifa mbalimbali pale wanapoona kuna jambo haliko sawa, hatua ambazo zimeibua hisia mseto kuhusu kuwajibika kwa viongozi katika mataifa wanayoyaongoza.

Maandamano hayo yamekuwa yakitekelezwa chini ya mwamvuli wa amani lakini katika mataifa kama Kenya na Bangladesh yamezua taharuki hali inayosababisha polisi kutumia nguvu kubwa katika hatua ya kukabiliana na waandamanaji.

Mandamano mengi yanayoanzishwa yakiitwa ya amani yamekuwa yakisababisha madhara makubwa kwa jamii ikiwamo vifo pamoja na vilema vya kudumu kwa wananchi na uharibifu wa mali na kutishia hatima ya biashara.

Aidha, yanasababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara, majengo, watu kupoteza mali, kufunga biashara pamoja na kusababisha umasikini miongoni mwa wanajamii, matokeo ambayo ni tofauti na dhamira ya kuanzishwa kwa maandamano.

Aidha, miongoni mwa mataifa ambayo migomo na maandamano yamekuwa kimbilio la wananchi katika hatua ya kuhamasisha kuwajibisha serikali ni Tanzania, ambako Juni 24, mwaka huu wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo jijini Dar es Salaam, waligoma kufungua maduka wakishinikiza serikali kutekeleza makubaliano yao waliyokubaliana mwaka 2023 katika kikao chao na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Baadhi ya wafanyabiashara wanasema, sababu kubwa iliyosababisha kufanya mgomo huo katika Soko la Kariakoo ni Mamlaka ya Mapato (TRA) kurudisha kikosi kazi zaidi kuliko ya awali iliyozuiliwa na Waziri Mkuu katika mkutano wa mwisho baina yao na serikali uliofanyika Mei, 2023 katika viwanja vya Mnazi Mmoja.

Baada ya mgomo huo uliodumu kwa siku nne na kusababisha hasara kwa wajasiriamali hao na serikalini kwa kupoteza mapato, haukuishia hapo bali ulifuatia kwa wafanyabiashara wa mikoa ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Mtwara na Mwanza.

Kutokana na hali hiyo, Waziri Mkuu Majaliwa alikutana na viongozi wa jumuiya ya wafanyabiashara na kupata suluhu ya tatizo hilo, hatua iliyosaidia wajasiriamali hao kufungua biashara zao.

**NIGERIA**

Kwa upande wa Nigeria takriban watu 13 walifariki wakati wa maandamano ya kupinga uongozi waliouita ni utawala mbaya na kupanda kwa gharama ya maisha, huku shirika lisilo la kiserikali la kutetea haki za binadamu, Amnesty International, likishutumu polisi kwa kuwaua waandamanaji walioandamana kwa amani.

"Ushahidi wetu, katika hatua hii, unaonesha kwamba pale palipokuwa na vifo, askari wa usalama walitumia mbinu za makusudi kuuwa wakati wakikabiliana na mikusanyiko ya watu wanaokemea njaa na umaskini mkubwa," ripoti ya shirika hilo iliyokaririwa na BBC, inasema.

Rais wa Nigeria Bola Tinubu, anaomba kusitishwa maandamano hayo yaliyodumu kwa siku tatu na kujitolea kufanya mazungumzo na waandamanaji, baada ya kuzuka ghasia mbaya na uporaji wa maduka na maghala.

**KENYA**

Nchini Kenya hali ilikuwa tofauti kidogo, baada ya Juni 20 mwaka huu maelfu ya vijana maarufu kama 'Gen Z' kuandamana wakishinikiza kuondolewa kwa mswada wa sheria ya fedha ya mwaka 2024/25 uliokuwa umeainisha kodi mpya zikiwamo kodi ya mkate, mazingira na kufafanua kuwa bidhaa zinazozalishwa nchini humo kama mayai zingetozwa kodi. Hata hivyo, mambo yalibadilika ikiwa zinazoagizwa nje ndizo zitakazotozwa kodi, kwa mujibu wa BBC.

Maandamano hayo yalizua taharuki baada ya kugeuka ghasia huku kuchoma magari, pikipiki, matairi barabarani, uvamizi wa ofisi za kiserikali na mihimili kama bunge na mahakama ikiwa ni moja ya matukio yaliyoshuhudia wakati wa mchakamchaka huo.

Kutokana na hali hiyo ilisababisha polisi kutumia nguvu ya ziada kukomesha maandamano hayo, jambo lililosababisha madhara kwa waandamanaji, vifo na majeruhi.

Hadi sasa serikali inasema kuwa, idadi ya waandamanaji waliopoteza maisha kutokana na maandamano hayo ni 25, huku takwimu za Shirika la Kitaifa la Kutetea Haki za Binadamu (KNCHR), zikielezea kuwa mauaji ya watu 41 na majeruhi ni 360.

Kutotana na shinikizo la Gen Z kuchukua sura mpya, Rais William Ruto, alichukua hatua ya kukataa kusaini mswada huo na kuamuru upitiwe upya huku akienda mbali zaidi ka kuamua kuvunja baraza lake la mawaziri na kuliunda upya.

Haikuishia hapo Julai 24, mwaka huu waandishi wa habari pia waliandamana wakipinga ukatili dhidi yao wakidai polisi waliowafyatulia Gen Z risasi wawajibishwe. Wanahabari walieleza kuwa wamepigwa, kutekwa nyara na kunyanyaswa wakati wa kuripoti maandamano ya Gen Z.

**UGANDA**

Julai 22, mwaka huu, nchini Uganda hali ilikuwa tofauti baada ya Rais Yoweri Museveni, kutoa onyo kali kwa wapinzani walioitisha maandamano ya kupinga ufisadi, akiwaonya kuwa wanacheza na moto. Nao, wakaonesha msimamo wa kuendelea licha ya vitisho dhidi yao.

Kutokana na hali hiyo wabunge watatu wa upinzani pamoja na watu wengine saba, walikamatwa na kufikishwa mahakamani na kushitakiwa kwa makosa mbalimbali ikiwamo kushiriki kwenye mkesha wa maandamano dhidi ya ufisadi yaliyopigwa marufuku.

Kiongozi mkuu wa upinzani nchini humo Bobi Wine, anaiambia BBC kuwa, wabunge Francis Zaake, Charles Tebandeke na Hassan Kirumira, ni sehemu ya Jukwaa la Umoja wa Kitaifa wa Chama cha NUP, ambao majengo yake yalizingirwa na polisi na wanajeshi waliokuwa na silaha.

**BANGLADESH**

Bangladesh pia ni mataifa yaliyokumbwa na mtafaruku mkubwa baada ya wanafunzi wa vyuo vikuu na vijana mbalimbali kuandamana wakipinga mfumo wa serikali katika utaratibu wa kutoa ajira, na kwamba hali hiyo ilisababisha watu 200 kupoteza maisha, inasema BBC.

Inaelezwa kuwa, waandamanaji hao walimshinikiza Waziri Mkuu Sheikh Hasina kuachia ngazi, hali iliyosababisha kujiuzulu na kukimbia nchini yake na kwenda uhamishoni, baada ya miaka 15 ya utawala wake.

Inaelezwa kuwa, kutokana na hatua ya kiongozi huyo kulikimbia taifa, hivyo sasa kumeundwa serikali ya mpito itakayosimamiwa na mshindi wa Tuzo ya Nobel Muhammad Yunus.

Hata hivyo, wachambuzi wa masuala ya kisiasa wanaeleza kuwa kuenea kwa migomo na maandamano katika maeneo mbalimbali duniani yakitumiwa na jamii kama nyenzo ya kuchochea kuwawajibisha viongozi, inapaswa kuchukuliwa kama kipimo na kujifanyia tathimini ya utendaji wao badala ya kutumia nguvu kujitetea.

Vilevile, wanasisitiza viongozi wa kisiasa kutumia hali hizo katika kujiimarisha kiutendaji kwa kufanyia kazi kikamilifu matatizo ya wananchi na kuhakikisha hayajirudii ili kujjengea imani kwa wapigakura wao badala ya kutegemea polisi na majeshi kuwashambulia raia huku wakiendelea kulalamikiwa.

KUELEKEA UCHAGUZI

# Cha muhimu ni maendeleo na si maneno, ahadi zisizotekelezeka

Na Dk Felician B Kilahama

KATIBA iliyopo, inaelekeza kuwa, kila ifikapo Oktoba baada ya miaka mitano ni uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani kwa Tanzania Bara wakati Visiwani Zanzibar wanaochaguliwa ni rais, wabunge, wawakilishi na madiwani.

Uzoefu unaonyesha kuwa nyakati za uchaguzi harakati zinakuwa nyingi na wagombea wanajaribu kadri wawezavyo kujinadi kwa mbwembwe na kutoa ahadi lukuki.

Kwa mtazamo mwingine, maneno ya wagombea yanakuwa ni ya kuwavitia wapigakura, ili mradi wachaguliwe kwa kwa kura nyingi kuliko wenzake.

Lakini licha ya ahadi hizo tamu wapigakura wengi hawana elimu ya kutosha kuchambua na kutenganisha 'yanayowezekana' na 'yasiyowezekana' kutekelezwa ndani ya miaka mitano kama wanavyoomba wagombea. Katika hali ya kawaida 'kudanganya' huwa ni kwingi kuliko uhalisia.

Wapigakura wengi hawana maarifa kujiuliza hivi wanasiasa kupitia ahadi au maneno ya matumaini, utekelezaji wa kile wanachokisema utakuwa vipi na kwa kutumia uwezo gani?

Kwa miaka zaidi ya 60 hatujiulizi kwa nini wanasiasa hawawi wakweli na kutuahidi yanayowezekana kuyatimiza kulingana na uwezo uliopo?

Tumekuwa tukishuhudia kuongeza kodi kwa wapigakura, ipo pia kanuni iliyozoeleka kusema, 'taifa linakopesheka' kama mataifa mengine hivyo hakuna kuhofu. Sawa, tukope, lakini tukijiuliza tunakopa ili kufanya nini?

Kama ni kutekeleza kilichoahidiwa je, tulidhamiria kukopa au ahadi ilitolewa kuvutia wapigakura bila ya kushirikishwa katika kupanga na hatimaye kufanya maamuzi kama ni kuongeza kodi, kukopa au kutokopa?

Miaka 63 ya uhuru lakini bado kwa kiasi kikubwa tunajikuta katika mahangaiko makubwa kuliko ahadi ambazo zimekuwa zikitolewa takribani miaka 40 iliyopita.

Wakati tunapata uhuru Mwalimu Julius Nyerere, aliwahi kusema tulikuwa karibu sawa na mataifa mengine kiuchumi na kutoa mifano kadhaa kama vile China, Malaysia, Vietnam, Thailand, Indonesia na Philippine.

Sasa China imepaa mno kiuchumi na kimaendeleo na ndilo taifa lenye kupambana na mataifa yenye nguvu kubwa duniani kiuchumi lakini pia ikitoa misaada mingi kwa Tanzania. Je, imetumia miujiza gani mpaka ikaifikia hatua hiyo wakati sisi bado tunajikongoja?

Siyo kwamba hatujasogea, kiuhalisia tumesogea ukilinganisha na hali ilivyokuwa wakati tunajitawala 1961. Pamoja na hayo, ukilinganisha yale yote yaliyofanyika kwa kipindi cha miaka mitano ya awamu ya tano ni mengi na yenye kutoa hamasa kubwa kwa Watanzania kwamba tukidhamiria kufanya kweli.




Mwenyekiti wa CUF, Profesa Ibrahim Lipumba, akizungumza na wananchi wakati wa ufunguzi wa kampeni za chama hicho . **PICHA: CUF**

Afrika tunaweza kujiendeleza. Hata hivyo, udhaifu wa kujiona kwamba tuko nyuma na masikini unaturudisha nyuma lakini kiuhalisia hatuko hivyo. Ukweli tunaweza, tunachokihitaji ni viongozi walio mahiri na wenye kuachana na roho za kutafuta kujitajirisha kutipia uongozi.

Ukipita mitaani mijini na vijijini kilio ni maisha na hali ngumu, kulalamikia kuzorota kwa huduma za kijamii iwe ni maji, afya, elimu, usitawi wa jamii, kilimo, mazingira na utawala bora.

Hali inayoonekana kama bado tumo katika mahangaiko ya kila namna, ndiyo maana tunahitaji kuona, kupitia uchaguzi ujao wanapatikana viongozi wasiokuwa wa maneno mengi bali wenye nia na msukumo wa kutuletea maendeleo ya kweli.

Naipongeza na kuiunga mkono kauli ya Dk. Doto Biteko, Waziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu kwamba: "Watanzania wanataka umeme siyo maneno".

Hivyo, akaagiza TANESCO na Wakala wa Umeme Vijijini (REA) kufanya yaliyosahihi na kwa wakati ili nchi ipate umeme wa uhakika nyakati zote, usiku na mchana.

Watanzania tunahitaji maendeleo si kingine. Nilisikia kupitia chombo kimoja cha habari, wakihabarisha kuwa gari lilipofika kwenye kijiji kimojawapo huko Wilayani Ludewa mkoani Njombe, watoto walilikimbia na kujificha wakiogopa ni kitu gani hicho? Vilevile, watu wazima wakajazana kwa wingi wakishangilia kuona gari limefika kwa mara ya kwanza kijijini hapo tangu uhuru.

Wakatoa pongezi nyingi kwa mbunge lakini swali ni hili pamoja na Watanzania hao, vipo vijiji vingapi vyenye hali kama hiyo?

Mwaka 2010 nilifika Tanganyika-Masagati mkoani Morogoro. Kutoka Mlimba cha TAZARA, hadi eneo hilo ni takribani kilomita 50, lakini ilichukua taribani saa tatu kufika kutokana na barabara ilivyokuwa mbaya. Nyakati za masika walisema inakuwa shida kupata huduma ya aina yoyote. Wakati ule ilikuwa karibu miaka 50 tangu uhuru sijui sasa hali ikoje huenda kumefanyika kitu lakini pana ukosefu wa huduma za uhakika.

Mwaka 2011 nilitembelea baadhi ya maeneo mkoani Katavi, kufika Mpanda haikuwa shida, maana kutoka Sumbawanga jitihada za kuitengeneza barabara zilikuwa zikiendelea.

Lakini kufikia vijiji kadhaa, ilikuwa changamoto kubwa barabara hazikuwa rafiki. Nilitamani kufika Tanganyika, ikawa vigumu kutokana na changamoto za barabara.

Kwa kuwa sasa ni Halmashauri ya Tanganyika huenda mawasiliano yameboreshwa kwa kiasi fulani.

Mwaka 2017 na 2018 nilifika wilayani Mlele na sehemu ya Kitunda Machimboni wilayani Sikonge. Wakati huo barabara ya Mpanda hadi Tabora ilikuwa ikijengwa na niliona kazi nzuri iliyokuwa ikifanyika. Barabara hiyo imekamika na ni moja ya njia bora iliyojengwa tangu awamu ya tano na kufunguliwa rasmi na awamu ya sita.

Nashauri tujifunge mikanda serikali pia ibane matumizi na kuelekeza fedha nyingi zitumike kwa weledi mkubwa ili kuwafanyia kweli Watanzania.

Miundombinu iwe namba moja bila barabara za uhakika, vijiji vingi vitabaki duni wakati tunahesabiwa kuufikia uchumi wa kati wa viwanda kumbe ni kinadharia, wachache ndiyo wanaofaidi uchumi wa kati.

Kuna haja ya kupunguza ukubwa wa serikali kuu ili kuelekeza nguvu kwenye serikali za mitaa, ambako huko ndiko tunatakiwa kuuona uhalisia wa maendeleo ya kweli vijijini.

Rasilimali fedha, magari, pamoja na vitendeakazi mbalimbali na wataalamu wengi na nguvu zaidi ielekezwe kwenye halmashauri na kuwajibika ipasavyo hadi vijijini mpaka maendeleo yawafikie Watanzania huko waliko.

Kazi kubwa ya serikali kuu iwe kusimamia utekelezaji wa sera na sheria pamoja na kutoa miongozo inayostahili kufanikisha matumizi sahihi ya fedha za kodi.

Vilevile, kuratibu shughuli zote za kiuchumi ili tusilaliwe kimaslahi wakati wawekezaji wanatengeneza faida kubwa kila mwaka na kutuachia mapato kiduchu huku rasilimali nyingi zinapatikana hapa nchini ikiwepo nguvukazi. Wataalamu wa fani mbalimbali wajizatiti taaluma zao zinachangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya Watanzania wengi vijijini na mijini.

Hivyo, kukuza uchumi wenye mtazamo chanya kwa watanzania na siyo kwa walengwa wengineo.

Serikali iwezeshe kiuhalisia watafiti wa taaluma mbalimbali ili kupitia wataalamu wanaotoa ushauri wa uhakika unaotokana na matokeo ya tafiti na isiwe kwa maneno ya kisiasa bali ushauri wa kitaaluma ulingane na matokeo ya kazi za mikono ya wataalamu walobobea katika Taaluma mbalimbali.

Nashauri viongozi watarajiwa 2025 wawe ni wale wanaoweza kusoma alama za nyakati na kufahamu Watanzania wengi wanataka nini.

Hivyo walete maendeleo endelevu kwa kuzivaa nafsi za wapigakura na hatimaye kukidhi haja za mioyo ya wengi kuliko ya wachache.

Kila jitihada zifanyike kuhakikisha fedha zinatumika kwa madhumuni yaliyolenga kuwainua wengi kimaisha na vingozi ngazi zote, wasimamie bila hila wala kuwepo udhalimu.

Kinyume cha hapo hatua kali zichukuliwe kwa watakaonekana na kuthibitishwa kimifumo au kiutawala na kisheria bila kujali nafasi aliyonayo mhusika.

JUKWAA LA VIONGOZI

# ACT Wazalendo imerejea na zigo la kero za wananchi mikoani

## •Wachambuzi wa kisiasa waisifia

Na Sabato Kasika

VIGOGO wa chama cha ACT Wazalendo, wamekamilisha awamu ya kwanza ya ziara ya mikoa 22 na majimbo 125 ya Tanzania Bara, wakielezea kubaini mizigo inayowaelemea Watanzania.

Jukumu hilo lililoanza Julai 22 na kukamilishwa Agosti 17, Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Mahusiano na Umma, Shangwe Ayo, anaeleza.

Katika mazungumzo yake na Nipashe, Shangwe anasema, viongozi wameshuhudia kero nyingi zinazowakabili Watanzania, ambazo wanataka serikali izifanyie kazi haraka.

"Viongozi wetu wamebaini kuwa walengwa wa wenye sifa za kupata fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF), ili kuwanusuru ambao ni wanakaya maskini, hawapati, badala yake wanapewa wajanja wachache," anadai.

Anafafanua kuwa, kwa kawaida fedha hizo hutolewa kwa kaya maskini lakini wamekutana na wazee wahitaji ambao waliwafuata na kuwaambia hawajawahi kunufaika.

"Tumeambiwa kuwa, wanandikishwa majina lakini hawapati msaada. Tunaona hii ni aibu kwa viongozi wa maeneo hayo ambao wameshindwa kusimamia jukumu hili kiweledi," anasema.

Shangwe, anataja kero nyingine kuwa ni huduma za afya, kuwa ni duni na kwamba wajawazito wanapokwenda hospitali kujifungua wanatozwa zaidi ya Sh. 50,000 akieleza kuwa ni kupingana na sera ya afya inayoeleza wahudumiwe bure.

Aidha, maeneo mengi ya vijijini, umaskini wa kipato ni mkubwa, familia nyingi hazina uwezo wa kumudu milo mitatu, na kwamba kuwatoza kiasi hicho cha fedha ni kuwaumiza.

"Vilevile, hakuna huduma za maji safi na salama, lakini pia, kubambikiwa kesi na uchelewеshaji wa kutoa hukumu za kesi mbalimbali unazungumzwa," anasema Shangwe.

Mbali na hayo, anasema kuna malalamiko ya migogoro ya ardhi katika maeneo mengi ya vijijini, ambako wamekutana na uporaji wa ardhi unaofanywa kibabe ukihusisha baadhi ya viongozi wa umma kuwapa wawekezaji.

### WAZUIA MIKUTANO

Licha ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuondoa vyama vya upinzani kifungoni, Shangwe anagusia kuzuiwa kwa mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa.

Anasema kwamba katika ziara hiyo wamekwamishwa na baadhi ya wakuu wa wilaya na polisi kuwaambia kuwa mikutano hiyo imezuiliwa.

"Kwa ujumla wananchi hawako huru hata wanapotaka kupaza sauti kuhusu vitendo vya kunyimwa haki zao, wanatishiwa jambo ambalo tunadhani si la kufumbia macho," anasema.

Aidha, kiongozi huyo anasema, viongozi wameandika waliyoyakuta mikoani na kukabidhi kwenye baraza la mawaziri kivuli la chama ili lichukue hatua.

"Chama chetu kina baraza la mawaziri kivuli, ambalo limekamilika, kwa hiyo kila wizara imepewa malalamiko yanayolihusu, ili waziri apaze sauti kwa serikali, ichukue hatua za kutatua kero hizo," anasema.

### WANA HAKI KUKOSOA

Baadhi ya wachambuzi wa masuala ya kisiasa wamepongeza hatua ya ACT-Wazalendo wakisema kinachofanywa na chama hicho ni sahihi .

Mchambuzi wa siasa na kada wa CCM, Abdulkarim Atiki, anasema ni haki ya vyama vya upinzani kuonyesha chama tawala sehemu ambayo kuna makosa ili serikali ijirekebishe haraka iwezekanavyo.

"Vyama hivi ni kama kioo, hivyo CCM haina budi kutumia kioo hicho kujiona ni wapi haiko sawa ili irekebishe, kwa hiyo taarifa yao ni ya muhimu kwa chama tawala na serikali," anasema Atiki.

Anafafanua kuwa ukosoaji wa upinzani unaisaidia CCM kujirekebisha na pale inapobaini kuwa kinacholalamikiwa ni kweli ni njia ya kurekebisha kasoro.

"Ni imani yangu kwamba serikali ikifikishiwa taarifa hizo itazifanyia kazi ili kuwaodolea wananchi kero zinazowakabili katika sekta mbalimbali," anasema.

Naibu Katibu Mkuu wa CUF Bara, Magdalena Sakaya, anasema ipo haja kwa CCM kukaa pembeni na kuachia wengine waongoze.

Anasema, chama hakina jipya, badala yake kinatakiwa kipumzike, kwa maelezo kuwa kimeshachoka kinatakiwa kukaa pembeni.

"CCM anaimba mwingine, anacheza mwingine. Yaani kinazungumza vingine kinatenda vingine," anasema Magdalena.

Anasema, ACT Wazalendo imetaja madudu machache, na kwamba yapo mengi kwenye sekta mbalimbali ikiwamo ya afya.

"Ukiangalia kwenye huduma ya afya, mtu anakuwa na bima ya afya, lakini anaambiwa akanunue dawa, Sasa hiyo bima ina maana gani kwa mwananchi?" anahoji.

Anasema, njia ya kumaliza kero zinazoikabili nchi, ni wananchi kuchangua viongozi bora wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa na mkuu wa mwakani.

### KAZI INAENDELEA

Akitangaza ziara zaidi, Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Mahusiano na Umma, Shangwe Ayo, anasema wameanza kutembelea wananch

Julai 22 mwaka huu na kumaliza Agosti 17.

Aidha, kinachofuata ni awamu ya pili itakayoanza | mwezi ujao na watafika katika mikoa minne na kutembelea majimbo 88 yaliyobakia.



Kiongozi wa Chama cha ACT –Wazalendo, Dorothy Semu. **PICHA: MTANDAO**

> "Tumeambiwa kuwa, wanandikishwa majina lakini hawapati msaada. Tunaona hii ni aibu kwa viongozi wa maeneo hayo ambao wameshindwa kusimamia jukumu hili kiweledi," anasema.

"Lengo letu ni kuingiza wanachama wapya milioni 10 na kuhamasisha wanachama na Watanzania kwa ujumla, kujiandaa ya uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wa mwaka 2025," anasema Shangwe.

Anafafanua kuwa katika ziara ya kwanza, kiongozi wa chama hicho, Dorothy Semu, ametembelea majimbo 30 kwenye mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Singida na Manyara

"Makamu Mwenyekiti Bara Isihaka Mchinjita, ameyafikia majimbo 28 kwenye mikoa ya Ruvuma, mkoa wa kichama wa Selous, Mtwara, Lindi, Pwani na Tanga," anasema.

Aidha, Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu ametembelea majimbo 21 katika mikoa ya Mwanza, Simiyu, Mara, Geita na Kagera, huku Kiongozi wa Chama Mstaafu Zitto Kabwe akizuru majimbo 36.

"Majimbo hayo 36 ni katika mikoa ya Kigoma, Rukwa, Katavi, Tabora, mikoa ya kichama Kahama na Shinyanga, pia katika ziara hiyo, viongozi wetu walizindua mpango wa kusajili wanachama wapya milioni 10 ndani ya miezi 10 kuanzia Julai 2024 na Aprili 2025," anasema.

Lengo lao ni kusikiliza kero mbalimbali za wananchi za kiuchumi, kijamii na kisiasa, kuzipazia sauti na kwamba hilo limefanyika kwa ufanisi.

Mbali na hayo, anasema, viongozi wamehamasisha Watanzania kujiandikisha kwenye rejista ya wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu 2025 ili chama hicho kipate ushindi.

"Tunawakaribisha Watanzania wote wajiandae kushiriki ziara yetu ya awamu ya pili kama walivyofanya katika ziara ya awamu ya kwanza wakatukabidhi kero zao. Tunaamini kwamba, kwa pamoja, tutaijenga Tanzania kwa maslahi ya wote," anasema Dorothy.



# TIRA yatangazia kiama wadanyangifu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imesema itawachukulia hatua watu watakaobainika kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu baada ya kughushi malipo ya mali na vyombo vya moto.

Kamishana wa TIRA, Baghayo Saqware, alitoa kauli hiyo juzi kwa waandishi wa habari kuhusiana na huduma zinazotolewa na Mamlaka hiyo wakati wa Uzinduzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani kitaifa inayofanyika jijini hapa.

Saqware, alisema jamii inapaswa kuacha udanganyifu katika uharibifu wa mali ili waweze kulipwa na bima kama fidia kitendo ambacho ni sawa na wizi

"Watu wengi wamekuwa wakisema uongo ili waweze kulipwa bima kitu ambacho hakitakiwi, watakaobainika watachukuliwa hatua kali za kisheria," alionya.

Aliwashauri wananchi kupata uhakika wa vyombo vya moto wanavyopanda kama vimekatiwa bima ili waweze kuwa na kinga endapo ajali itatokea.

Saqware, alisema wananchi wanapaswa kufanya hivyo ili kujihakikishia usalama wao wa safari wanazofanya kwa kutumia vyombo hivyo.

Alisema kazi ya mamlaka hiyo ni ni kuhakikisha bidhaa za bima zinawafikia walengwa na kutumiwa ipasavyo kwa maendeleo endelevu.

# Watakiwa kukemea ushoga, usagaji

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, Asia Messos amewataka wananchi wilayani hapa kukemea ushoga na usagaji ili kudhibiti mmomonyoko wa maadili katika jamii yao.

Messos, alitoa wito huo juzi wakati wa ziara ya kusikiliza na kutatua kero zinazowakabili wakazi wa vijiji vya Gumanga na Nduguti.

Messos, wakazi hao wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kupinga mila na desturi zinachochea mmomonyoko wa maadili katika jamii.

"Tujikite katika malezi yetu, turudi katika misingi yetu ya Kitanzania. Hii iwe ajenda katika mikutano yetu, nyumba zetu za ibada. Tuungane kupinga ushoga na usagaji katika jamii zetu," alisema.

Aliwataka wazazi kuwapeleka watoto wao shule kwa manufaa ya maisha ya baadaye na kuchangia chakula shuleni.

Akizungumzia kuhusu uchaguzi wa serikali unaotarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu, aliwataka wakazi hao kujitokeza kwa wingi ili wachague viongozi bora.

"Nawasihi msipoteze haki zenu za msingi, utakapofika wakati wa kujiandikisha, mjiandikishe, utakapofika wakati wa kampeni jitokeze na itakapofika wakati wa kupiga kura tujitokeze kuwachagua viongozi wetu tunaowataka," alisema Messos .

Awali akielezea mambo makubwa yaliyofanywa na serikali katika miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan, Messos, alisema Mkalama imepokea zaidi ya Sh. bilioni 60 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya elimu, afya umeme, barabara na kilimo.

# 'Si dhambi viongozi wa dini kushiriki uchaguzi nchini'

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Karmali Assemblies of God Tanzania (K.A.G), Dk. Evance Chande amesema si dhambi viongozi wa dini nchini kushiriki mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu kwa sababu wana mchango wa kuhakikisha wananchi wanapata maendeleo.

Dk. Chande alitoa kauli hiyo juzi jijini hapa wakati akifungua semina ya kuwajengea uwezo wachungaji.

Askofu Chande, alisema kwa viongozi hao kushiriki mikutano ya kampeni za uchaguzi huo siyo dhambi kwa kuwa wanatakiwa kuchagua viongozi wanaowaona wanafaa kuongoza wananchi ambao ni waumini wao.

"Siasa ndiyo zinazowaweka madarakani viongozi wote wa siasa ambao ndiyo wanaotupa hata sisi uhuru wa kuabudu, hivyo ninawaomba wasijitenge kwa kukaa mbali, bali waende kushiriki kwenye mikutano hiyo ya siasa," alisema na kusisitiza kuwa:

"Kushiriki mikutano ya siasa na hata uchaguzi wa serikali za mitaa siyo dhambi, ukiangalia hata viongozi wetu, rais,wabunge madiwani na wenyeviti wetu wa serikali za mitaa na vijiji wote hao wametoka kwenye siasa."

**"Siasa ndiyo zinazowaweka madarakani viongozi wote wa siasa ambao ndiyo wanaotupa hata sisi uhuru wa kuabudu, hivyo ninawaomba wasijitenge kwa kukaa mbali, bali waende**

Alisema viongozi wa dini ndiyo wanaoweza kuwachagua na kuwaweka madarakani wabunge na madiwani kupitia kura zao.

Kwa upande mwingine, Dk. Chande, aliwaomba viongozi wa dini kuwahamasisha waumini wao kujitokeza kujiandikisha wakati wa uboreshaji taarifa zao kwenye daftari la kudumu la wapigakura ili wapate fursa ya kuchagua viongozi katika uchaguzi huo na mkuu mwakani.

Katibu Mkuu wa Kanisa hilo, Bazoro Mtila, alisema wachungaji hao watajifunza uongozi, utatuzi wa migogoro na usimamizi wa fedha kwenye maeneo yao.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, mkoani Singida, Asia Messos (kulia), akizungumza na wakazi wa kijiji cha Gumanga juzi, wakati wa kikao cha kusikiliza na kutatua kero zinazowakabili. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# CCM wakomalia ujenzi wa maabara

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) wilayani hapa Mkoa wa Singida kimetoa mwezi mmoja kwa serikali kuhakikisha ujenzi wa maabara ya Shule ya Sekondari Kamenyanga unakamilika na kuanza kutumiwa na wanafunzi kwa maandalizi ya mitihani ya sayansi.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Manyoni, Jumanne Makhanda alitoa agizo hilo juzi baada ya Kamati ya Siasa ya Wilaya hiyo kukagua ujenzi wa maabara hiyo kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya chama hicho katika Kata ya Aghondi.

Makhanda, alisema ujenzi wa maabara hiyo ambayo serikali ilitoa Sh. milioni 30 unatakiwa kukamilika haraka ili wanafunzi hususani wa madarasa ya mitihani waweze kuitumia kwa ajili ya kujiandaa na mitihani hali itakayoongeza ufaulu wa masomo.

Alisema serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imetoa fedha nyingi katika wilaya hiyo kwa utekelezaji wa miradi ya sekta ya elimu, hivyo kinachotakiwa ni watendaji kusimamia na kukamilika ndani ya mkataba.

"Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutujali sana sisi Wilaya ya Manyoni, ametupa fedha nyingi sana, sasa watendaji tusimwangushe tuhakikishe miradi inakamilika kwa wakati," alisema Makhanda.

Awali Mkuu wa Shule ya Sekondari Kamenyanga, Anjendile Makweta akisoma taarifa ya utekelezaji wa miradi, alisema shule hiyo ilipokea Sh. milioni 42.5 kwa ajili ya ujenzi wa maabara ya somo la Baolojia na ukamilishaji wa chumba kimoja cha darasa.

Makweta, alisema wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo, walichangia nguvu zao kwa kuchimba msingi na kujaza kifusi vyenye thamani ya Sh. 200,000.

Alisema ujenzi wa maabara hiyo umechelewa kukamilika baada ya fundi aliyepewa zabuni kufanya makosa wakati alikuwa amelipwa fedha zote.



HABARI MBEYA

# Shangazi, hawara yake mbaroni mauaji ya mtoto

Na Elizabeth John, NJOMBE

MTOTO Wilson Kipela, mwenye umri wa miaka mitano anadaiwa kuuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani na shanganzi yake na hawara yake kwa kushirikiana kwa kushirikiana kwa kile kinachohusishwa na imani za kishirikina.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga alisema kuwa mauaji hayo yalitokea juzi majira ya saa 11:30 alfajiri katika Mtaa wa Mapinduzi ya Kijani.

Banga,

Banga alisema wanawashikilia watuhumiwa hao kwa tuhuma za mauaji ya mtoto huyo baada ya kutoka kunywa pombe usiku.

Kamanda huyo, alisema licha ya watuhumiwa hao kushirikiana katika tukio hilo, mtu wa mwisho ambaye amekutwa akimalizia ni Furahini.

Alisema jeshi hilo linaendelea na uchunguzi wa mauaji hayo kutokana na kudaiwa kuhusishwa na imani za kishirikina.

Kamanda huyo, alisema baba yake mzazi mtoto huyo alifariki mwaka jana kwa ajali na alikuwa akiishi na bibi yake Igwachanya, lakini aliletwa Makambako kupatiwa matibabu kwa bibi yake mwingine na ndipo shangazi yake huyo alipomchukua.

"Sasa tarehe 25 (Agosti) walimchukua huyo mtoto wakiwa na hawara yake na kwenda naye katika kilabu cha pombe,

**"Sasa tarehe 25 (Agosti) walimchukua huyo mtoto wakiwa na hawara yake na kwenda naye katika kilabu cha pombe, wakanywa pombe huko wakati wanarudi nyumbani usiku...**

wakanywa pombe huko wakati wanarudi nyumbani usiku wa manane ndipo walipoanza kumpiga huyo mtoto wakiwa katika ulevi uliopindukia na kumkanyaga kwa miguu," alisema Banga.

Alisema watuhumiwa hao watarajiwa kufikishwa mahakamani kujibu mashtaka ya mauaji baada ya upelelezi kukamilika.

"Mimi siamini kama ni pombe, mimi naamini ni imani za kishirikina kwa sababu hauwezi kumuua mtoto ambaye hajakukosea jambo la aina yoyote hata kama pombe kwa hiyo tunaendelea kuchunguza hili jambo na mwisho wa siku tupate ukweli halisi," alisema.

Alitoa wito kwa wananchi mkoani hapa kupunguza unywaji wa pombe na kuacha kwenda na watoto katika maeneo ya vilabuni na baa.

Mwenyekiti wa Mtaa huo, John Mligo, aliliambia Nipashe baada ya kupata taarifa za mauaji hayo, alifika nyumbani kwa watuhumiwa hao na kukuta wakiwa na chupa mbili za bia huku wamelewa.

Mmoja wa wakazi wa mtaa huo, Rehema Sengele, alidai usiku wa manane wakati mwanamke huyo ametoka kunywa pombe akiwa na mtoto huyo, baada ya kufika nyumbani alianza kumpiga na kumsababishia majeraha kichwani kisha mauti.




Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim Tanzania, Stanley Kafu (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu Tamasha la Exim Bima 2024, likiwa lenye kaulimbiu ya 'Amsha Matumaini', linalotarajiwa kufanyika Septemba 28 mwaka huu katika viwanja vya Gymkhana. Kushoto ni Meneja wa Idara ya Bima ya benki hiyo, Tike Mwakyoma na Meneja Mkuu kutoka Idara ya Masoko na Mawasiliano, Kauthar D'souza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vituo vya huduma ya tohara vyapatiwa vishikwambi

Na Gideon Mwakanosya, RUVUMA

VITUO 43 vya afya vinavyotoa huduma ya tohara mkoani hapa vimekabidhiwa vishikwambi 84 vyenye thamani ya shilingi milioni 39 kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi kwa wananchi.

Akizungumza juzi kabla ya kukabidhiwa vishikwambi hivyo, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Dk. Louis Chomboko, alisema vimetolewa kusaidia kutekeleza afua ya tohara kinga kwa wanaume na kuzuia maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) kwa asilimia 60.

"Vishikwambi hivi vimekuja wakati mwafaka na sasa vitaenda kugawiwa kwa vituo 43 kwa watoa huduma na waelimishaji rika ili kukusanya takwimu ya wale wote ambao tutakuwa tunawafikia kwa huduma ya tohara," alisema Dk. Chomboko.

Alibainisha kuwa Mkoa wa Ruvuma unashirikiana na Taasisi ya HJF Medical Research International ambayo imetoa vishikwambi hivyo ili kuwezesha ufuatiliaji.

Mwakilishi wa taasisi hiyo ambaye pia ni Msimamizi wa Tohara wa Mkoa huo, Dk. Joshua Mwakanyamale, alisema inafanya kazi katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ya Mbeya, Rukwa, Songwe, Ruvuma na Katavi.

Dk. Mwakanyamale, alisema vishikwambi hivyo vitarahisisha utunzaji wa taarifa na kumbukumbu tofauti na ule wa karatasi.

# Hapi: Acheni kutembea na majina ya wagombea mfukoni

Na Elizabeth John, NJOMBE

VIONGOZI wa jumuiya za Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamewatakiwa kushikamana na kuacha kutembea na majina ya wagombea mifukoni badala yake wahamasishe wananchi kujiunga na chama hicho ili kipate ushindi katika uchaguzi ujao nchini.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi wa CCM Taifa, Ally Hapi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika Jimbo la Lupembe Wilaya ya Njombe, ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya siku tatu mkoani hapa ya kukutana na wanachama na kukagua uhai wa chama hicho.

Alisema viongozi wa jumuiya hizo wanatakiwa kuwafikia wanachama hadi kwenye ngazi za mashina ili kuwaeleza kazi nzuri zinazofanywa na serikali ya awamu ya sita.

Alisema pia wanatakiwa kuhamasisha wanachama wa chama hicho kujitokeza kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura na kugombea nafasi katika uchaguzi wa serikali za mitaa Novemba mwaka huu na mkuu mwakani.

"Mnatakiwa kujipanga ili kushinda katika chaguzi za serikali za mitaa na uchaguzi mkuu kwa kusajili wanachama wapya na kufanya mikutano ya kata, matawi na shina," alisema Hapi.

Hata hivyo, alisema kazi ya kutafuta kura inahitaji kutoka na si kukaa ofisini ili kuwafikia wanachama, kuzungumza nao na kuwahamasisha kwenda kupiga kura. Hapi aliwasihi wanachama hao kuepuka makundi ya kukigawa na kukidhoofisha chama na badala yake washikamane kwa kuwa wamoja na kuacha kutembea na wagombea mfukoni.

"Acheni kuwa na wagombea mifukoni na kupokea miamala kutoka kwa wagombea ambayo ndio inawavuruga, kataeni kuwa chawa wa mtu," alisisitiza Hapi.

Awali, Hapo, alisema serikali inaendelea kuboresha mradi wa umeme wa Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere na reli ya SGR nchini ili kuboresha huduma kwa wananchi.

Alisema serikali inatarajia kutumia takribani Sh. trilioni 24 hadi kukamilika reli ya SGR, mradi huo ambao utafika nchi za Rwanda na Jamhuri ya Demokrasia Congo (DRC).

Alisema kiasi kingine shilingi trilioni saba kitatumika kukamilisha ujenzi wa mradi wa bwawa la umeme la Mwalimu Julius Nyerere ambao umefika zaidi ya asilimia 90 na kupunguza changamoto ya kukatika katika nishati hiyo nchini.

"Wana CCM mna kila sababu ya kumsifu, kumpongeza na kumuunga mkono Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa sababu ya utendaji wake, busara zake na uwezo wake wa kuendeleza miradi viporo iliyoachwa na mtangulizi wake Hayati Dk. John Pombe Magufuli," alisema.

Mbunge wa Lupembe, Edwin Swalle, alisema serikali imetekeleza miradi mingi ya maendeleo katika jimbo hilo, ikiwemo ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na shule na kuwaondolea adha wananchi kutembea umbali mrefu kufuata huduma.

# TAKUKURU, ZAECA zatakiwa kushirikiana

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), zimetakiwa kuongeza ushirikiano ili kuleta mafanikio katika miradi ya kimkakati inayotekelezwa nchini.

Wito huo ulitolewa Ikulu jana na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi wakati akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Crispin Francis Chalamila alipofika kujitambulisha baada ya kuteuliwa kushika wadhifa huo na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan hivi karibuni.

Dk. Mwinyi, alisema amezishauri taasisi hizo kuzidisha ushirikiano hasa kwenye miradi ya kimkakati ya mendeleo kwa maslahi ya taifa.

Alimpongeza Chalamila kwa uteuzi huo na kumtakia heri kwenye majukumu yake mapya.

Vilevile, aliisifu ZAECA kwa kutekeleza kwa ufanisi makujukumu yao hasa kwenye miradi ya serikali.

Kwa upande wake, Chalamila alimuahidi Dk. Mwinyi kuendeleza ushirikiano uliopo baina ya ZAECA na TAKUKURU ili kufanikisha majukumu yao.

Alisema TAKUKURU na ZAECA wanashirikiana kwenye mambo mengi tangu kusaini mkataba wa ushirikiano wao wa mwaka 2012 uliolenga kujengeana uwezo, uchunguzi na kushiriki mikutano ya pamoja ya kikanda na kitaifa.

Chalamila alipongeza maendeleo yaliyofikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais Dk. Mwinyi.

# Serikali yasisitiza kuwekeza sekta ya elimu Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesisitiza kuwa serikali itaendelea kuwekeza zaidi katika sekta ya elimu kwa ujenzi wa miundombinu ili kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi kila mwaka.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo katika viwanja vya Ikulu Mjini Unguja kwenye hafla maalum ya chakula cha mchana aliyowaandalia wanafunzi wa kidato cha nne na cha sita waliofanya vizuri katika mitihani yao ya taifa ya mwaka jana kwa kidato cha nne na mwaka huu cha sita kwa Unguja.

Dk. Mwinyi alisema amefarijika na mafanikio yaliyopatikana kufuatia idadi ya wanafunzi waliopata daraja la kwanza kuongezeka.

Alisema serikali itaweka kipaumbele kuimarisha miundombinu, kuajiri walimu zaidi hasa kwa masomo ya sayansi na kusimamia maslahi ya walimu ili kuwaongezea motisha wa kufanya kazi.

Alisema serikali inatarajia kuongeza fedha za mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya juu na kutoa wito kwa wanafunzi kutumia fursa hiyo kujiendeleza zaidi kielimu.

**Dk. Mwinyi, alisema elimu ni sekta ambayo matokeo yake hayaonekani mara moja, lakini kasi inayoendelea kwa sasa hususani kwa wanafunzi wa Zanzibar inatia moyo na**

Dk. Mwinyi, alisema elimu ni sekta ambayo matokeo yake hayaonekani mara moja, lakini kasi inayoendelea kwa sasa hususani kwa wanafunzi wa Zanzibar inatia moyo na kuishawishi serikali kuwekeza mkazo zaidi kuwekeza katika elimu.

Aliwahakikishia wanafunzi kuwa utaratibu wa kuwapongeza, kuwapa zawadi na kula pamoja nao utaendelea kila mwaka kwa dhamira ya kuwapa hamasa ya kusoma kwa bidii na kufaulu.

Dk. Mwinyi aliwataka wanafunzi kutobweteka na mafanikio waliyoyapata bali wasome zaidi ili kufikia elimu ya juu na kuwapongeza wanafunzi saba waliopata matokeo ya alama A3 katika mitihani yao.

Alisema amefarajika na kazi kubwa inayofanywa na walimu na kuwa kichocheo cha mafanikio yanayopatikana kwa sasa.

Alizipongeza serikali za wilaya na mikoa kwa kuendelea kusimamia ipasavyo sekta ya elimu na kuchangia kuleta mafanikio.

Akizungumza katika hafla hiyo, Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alisema mafanikio yanayopatikana katika elimu ni juhudi za Dk. Mwinyi kuwekeza katika sekta hiyo na kuahidi kuziunga mkono.

Abdulla, alisema maono yake katika kuimarisha miundombinu ya elimu yameleta utulivu na kuwafanya wanafuzi kusoma kwa bidii wakiwa katika miundombinu bora na ya kisasa inayomvutia kila mwanafunzi.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia wa Tanzania, Profesa Amosi Nkenda, alisifu mabadiliko makubwa yanayofikiwa na Zanzibar katika ukuaji wa elimu na kupongeza kazi inayofanywa na Rais Mwinyi.

Mkenda, alisema seriklai imeongeza bajeti katika mikopo ya elimu ya juu kutoka Sh. bilioni 4.64 hadi kufikia Sh. bilioni 7.57 ili kuwawezesha wanafunzi wengi zaidi kujiunga na elimu ya juu.

Wanafunzi wote waliofanya mitihani ya kidato cha nne mwaka jana kwa shule za Zanzibari walikuwa 24, 420 kati ya hao Unguja 16, 771, waliofaulu na kupata daraja la kwanza ni 958.

Kidato cha sita 3,402, kwa Unguja 2,358, waliofaulu na kupata daraja la kwanza ni 594.

Wanafunzi wawili, Mwanaarabu Said Ibrahim kutoka Shule ya Sekondari Lumumba, Ilham Abdalla Awadh wa Fedha Zanzibar na wenzao watatu kutoka Tanzania Bara, waliwakilisha Tanzania nchini Afrika Kusini kwenye mashindano ya Hisabati kwa Afrika nzima, walipata ushindi watatu.



Mamalishe wa soko la Msamvu, mjini Morogoro, Halima Kimairo ambaye ni mmoja wa wanufaika wa mpango wa ukopeshwaji wa nishati safi ya kupikia kutoka kampuni ya Taifa Gas, akiandaa chakula kwa ajili ya wateja wake sokoni hapo, juzi. Mkopo huo ni sehemu ya majaribio kuelekea utekelezaji wa mpango mkubwa wa kampuni hiyo unaolenga kutoa mikopo ya nishati hiyo kwa wajasiriamali 1000 katika mikoa yote nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachina kutokomeza kichocho Unguja, Pemba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema itaendelea kushirikiana na China kupambana na maradhi ya kichocho katika jamii hususani kisiwani Pemba.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui katika hafla ya kuaga timu ya kwanza ya wataalamu wa kichocho baada ya kumaliza muda wake wa kufanya kazi na kuikaribisha timu ya pili katika ofisi za ubalozi mdogo wa China zilizopo Mazizini visiwani hapa. Mazrui, alisema kazi kubwa inayofanywa na wataalamu hao wa China ni kutokomeza kichocho katika visiwa vya Unguja na Pemba na kwamba wameweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa. Alisema nchi hiyo kwa kushirikiana na wataalamu wa Zanzibar kupitia mradi wa China AID wamedhibiti maradhi hayo kutoka asilimia 8.92 hadi kufikia 0.64 kisiwani Pemba.

Waziri huyo, alisema Serikali ya Zanzibar kupitia wizara hiyo itaendelea kushirikiana na China kuimarisha huduma kwa wananchi wa visiwa hivyo.

Kaimu Balozi mdogo wa China, Zhang Ming, alisema nchi yake, itaendelea kuimarisha huduma za afya, ikiwamo kutokomeza kichocho hasa Pemba kutokana na takwimu kuonesha kukithiri kwa ugonjwa huo. Alisema wataalamu wa kichocho kwa awamu ya pili, wataendelea kuchukua jitihada kisiwani humo kudhibiti maradhi hayo yasiendelee na kuathiri wakazi wake. Kiongozi wa mradi huo, Dk. Yuzheng Huang ambaye amemaliza muda wa kufanya kazi Zanzibar, alisema wametoa elimu dhidi ya kichocho kwa wanafunzi shuleni, jamii na kuwapatia matibabu wenye vimelea vya ugonjwa huo.

Kongozi mpya wa timu ya kupambana na kichocho visiwani hapa, Dai Yang, alisema wataendelea kudhibiti maradhi hayo kwa kutoa elimu kwa jamii na huduma za afya

Mratibu wa magonjwa yasiyopewa kipaumbele Pemba, Saleh Juma, alisema jitihada zilizofanyika zimesaidia kupunguza kichocho kisiwani humo.

Alisema katika kupambana na maradhi hayo, walipita shehia zote na shule na waliobainika kuambukizwa walipatiwa matibabu.

HABARI KITAIFA

# Watatu wahukumiwa kunyongwa hadi kufa mauaji Mirembe, GGM

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania, Kanda ya Geita, imewahukumu watu watatu kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua Mirembe Seleiman Hungwe aliyekuwa mfanyakazi wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML).

Katika tukio hilo, washtakiwa hao walimcharanga mapanga shingoni, kichwani na kukata kiganja cha mkono wake wa kulia na kufariki dunia papo hapo, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

Waliohukumiwa ni Dayfath Maunga (30), mkazi wa Usagara, Safari Bundala (54), mkazi wa Chigunga na Geja Deus (30), mkazi wa Bugarama.

Hukumu hiyo imetolewa jana na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Kevin Mhina, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipokuacha shaka yoyote.

Jaji Mhina alisema mahakama hii inatoa adhabu kali dhidi ya washtakiwa hao ili iwe fundisho kwao na kwa watu wengine wenye tabia za kikatili kama zao.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Scolastica Teffe, ambaye alipeleka mahakamani hapo mashahidi 29 na vielelezo 18, ambavyo vilithibitisha kuwa washtakiwa walitenda kosa hilo la mauaji.

Aidha, Jaji Mhina alisema mshtakiwa wa tatu ndiye aliyebainisha mauaji ya Mirembe kwa kuonesha panga na simu moja ya marehemu mirembe.

Alisema mshtakiwa wa tatu wakati akiandikwa maelezo yake ya onyo, alikiri kuhusika na mauaji ya Mirembe, kwa kusema alipochuchumaa alimkata panga kichwani, shingoni na kukata kiganja cha mkono wa kulia.

Alisema baada ya mshtakiwa huyo kukiri kosa hilo, aliwapeleka polisi sehemu alipokuwa ameficha panga (jambia) likiwa na damu pamoja na simu moja ya Mirembe ambayo alikuwa ameitupa chooni.

Jaji Mhina alisema mshtakiwa wa kwanza na wa pili, hao ndiyo walipanga njama ya kumuua marehemu Mirembe, mshtakiwa wa pili alikwenda kwa waganga wa kienyeji ili kumroga (Mirembe), lakini haikuwezekana ndipo akaamua kutafuta wauaji ili waweze kumuua kwa dau la Sh. milioni 2.6.

Alisema chanzo cha kifo chake ni kutokwa kwa damu nyingi baada ya kupata majeraha makubwa matatu yenye setimeta 14, 8 na 6 ambaya yalikuwa shingoni, kichwani na ya kutokana na kukatwa kiganja cha mkono wake wa kulia.

Jaji Mhina alisema mshtakiwa wa kwanza ndiye alikuwa akiishi na Mirembe na katika maelezo yake ya onyo, mshtakiwa huyo alikiri kuhusika na mauaji hayo kwa madai kuwa alikuwa anampiga, anamnyanyasa na alipopanga kuondoka, alimkataza ndipo akaamua kutafuta wauaji ili aweze kuwa huru.

Alisema mshtakiwa wa kwanza ndiye aliyebainisha washtakiwa wa pili na wa tatu kukamatwa.

Jaji Mhina alisema upande wa mashtaka umethibitisha kosa hilo pasipo kuacha shaka yoyote na mahakama imewatia hatiani mshtakiwa wa kwanza, wapili na watatu.

"Katika sheria za nchi yetu watu wanaobainika katika kesi ya mauaji hukumu yao ni kunyongwa hadi kufa," alisema Jaji Mhina.

**Alisema baada ya mshtakiwa huyo kukiri kosa hilo, aliwapeleka polisi sehemu alipokuwa ameficha panga (jambia) likiwa na damu pamoja na simu moja ya Mirembe ambayo alikuwa ameitupa chooni.**

Upande wa utetezi wa washtakiwa ulikuwa ukiongozwa na mawakili watatu wa kujitegemea ambao ni Erick Lutahanga, Laurent Bugoti na Elizabeth Msechu, kwa pamoja waliiomba mahakama itowe adhabu kwa washtakiwa kwa mujibu wa sheria.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Teffe, aliomba mahakama hiyo itowe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Jaji Mhina alisema mahakama hiyo inawahukumu mshtakiwa wa kwanza, wapili na watatu kunyongwa hadi kufa na haki ya rufani ipo wazi.

Katika kesi hiyo, washtakiwa walikuwa wanne ambao ni Dayfath Maunga, Safari Bundala, Genja Deus na Mussa Pastory, mshtakiwa wa nne Mussa Pastory (33), mkazi wa Bulyanhulu Msalala, Shinyanga, aliachiwa huru.

Awali, akisoma hati ya mashtaka, Karani wa Mahakama hiyo, Felister Mlolwa, alidai mahakamani hapo kuwa Aprili 26, mwaka huu, katika maeneo ya Mwatulole Mkoa wa Geita, washtakiwa wote kwa pamoja waliimuua Mirembe aliyekuwa mfanyakazi wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kumcharanga mapanga shingoni, kichwani na kukata kiganja cha mkono wake wa kulia na kufariki dunia papo hapo, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

Wakati hukumu hiyo ikitolewa umati wa wananchi ulifulika mahakamani hapo wakiwamo ndugu wa marehemu Mirembe pamoja na ndugu wa washtakiwa, kushuhudia hukumu hiyo ambayo imesomwa kwa muda wa saa tatu kuanzia saa 3 asubuhi hadi saa 6 mchana.

# Makalla ataja siri ya ushindi CCM kuelekea uchaguzi mitaa

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla, amesema chama hicho kinategemea viongozi wa mashina, matawi na mabalozi katika kushinda uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji unaotarajiwa kufanyika Novemba 27 mwaka huu.

Alisema hayo jana Kigamboni, Dar es Salaam, wakati akizindua Shina la Wakereketwa Wavuvi Beach Mjimwema, ikiwa ni sehemu ya ziara ya siku tatu aliyoianza wilayani humo.

Agosti 19 mwaka huu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohammed Mchengerwa, alitangaza tarehe rasmi ya uchaguzi huo, akisema utashirikisha vyama vya siasa 19 vyenye usajili wa kudumu.

Akizungumza na wanachama wa CCM wakati akizindua shina hilo, Makalla alisema kuelekea uchaguzi huo, CCM nguvu yake kubwa ipo katika viongozi hao ili kuibuka na ushindi.

Makalla aliwataka viongozi hao nchini kuhakikisha katika uchaguzi huo CCM kinaibuka na ushindi mkubwa na wa kishindo.

"CCM nguvu yake kubwa ipo katika viongozi wa mashina, matawi na mabalozi. Hivyo kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa tunawategemea sana viongozi hao. Pia CCM inategemea jumuiya zake ikiwemo Umoja wa Wanawake ( UWT) pamoja na Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi ( UVCCM) kupata wanachama," alisema.

Kadhalika alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Halima Bulembo, kuhakikisha mikopo ya asilimia 10 ya halmashauri itakapoanza kutolewa asiwasahau vijana wa CCM wa shina hilo.

"Vijana wajasiriamali wengine mnapaswa kuiga mfano wa shina hili walichokifanya. Pia tunatarajia ushindi mkubwa wa Serikali za Mitaa hapa Mjimwema kupitia shina hili," alisema Makalla.

Pamoja na mambo mengine, Makalla aliwachangia Sh. milioni moja wanachama wa CCM shina hilo ili iwasaidie katika shughuli za shina hilo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MOSHI**

**Kituo cha MOSHI MJINI Mkoa KILIMANJARO**
**Shauri la Ndoa Na. 102/2024**

**Jina la mdai: DISMAS MASALU DEDE**

**Jina la mdaiwa: AHMED HILAL**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Kwa: AHMED HILAL**
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba
Mdai anadai Tshs **4,000,000/=** ikiwa ni fedha ambayo alikutumia kwa bank ya CRDB kwa muhamala wa tarehe 22/08/2024 hivyo fika Mahakamani kujibu madai hayo.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 13 mwezi wa 09 Mwaka 2024 saa 4:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 27 Mwezi 08 Mwaka 2024.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MOSHI – MJINI

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT DELEGATED COURT OF MOROGORO**
**AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.53368 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE REUBEN RICHARD LEMA- DECEASED**
**AND IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATION BY**
**MONICA CHARLES NINDIE....................................PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Made under rule 75 of the probate and administration of Estate rule, CAP 352 R,E 2019)**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 29th day of 08,2024.
DATED and SIGNED at Morogoro this 21th day of 08,2024.

Senior Resident Magistrate
MOROGORO

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**RICHARD SATTERTHWAITE MABALA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya FORD KUGA yenye usajili namba **T 156 DSY**, CHASSIS NAMBA: **WF0AXXWPMADK63619** na ENGINE NAMBA: **DK63619.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/TEM/181752/2024**

**KATIBU BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOKO SONGEA**

**MAOMBI NAMBA 51/2024**

**ANDREA KISINGA ............................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**BEDA BEDA TAWETE .........................WAJIBU MAOMBI**
**EZEKIEL KILOWOKO**

**WITO/KUITWA SHAURI**

Ezekiel Kilowoko unataarifiwa kuwa Mleta Maombi amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako. Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako, au wote kwa pamoja siku ya tarehe 17/09/2024 saa 3: 00 Asubuhi. Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazni kwaajili ya kuleta hati zako za utetezi.
Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hii upande mmoja bila kujali uwepo wako.
Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 26/08/2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
SONGEA

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 14942 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late: MARIAM AMANI BIGAMBO**

**By 1: OBEDI MAJUNGU BIGAMBO**
**2: ________________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 11 day of 09.2024

Dated at MOROGORO this 26 day of 08.2024

RESIDENT MAGISTRATE

**KUPOTEA KWA CHETI**



**SALVINA A. MWUMBE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0209.0042** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KOROGWE GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/181652/2024.**

**HABARI KIMATAIFA**

## Idadi ya vifo vya mafuriko nchini Sudan vyafikia 132

**KHARTOUM,** Sudan

WIZARA ya Afya nchini Sudan imesema idadi ya vifo vinavyotokana na mafuriko yanayosababishwa na mvua kubwa inayoendelea kunyesha katika taifa hilo imefikia 132, huku watu 210 wakiwa hawajulikani waliko.

Taarifa hiyo ilitolewa jana, ikielezwa kuwa nchi hiyo imekumbwa na msimu wa mvua nyingi tangu mwezi uliopita, huku mafuriko ya hapa na pale yakiambatana hasa katika maeneo ya kaskazini na mashariki mwa taifa hilo.

"Majimbo yaliyoathiriwa ni 10, idadi ya familia zilizoathiriwa ilipanda hadi 31,666 na watu binafsi ni 129,650," ilisema sehemu ya taarifa hiyo. Wakati mafuriko yakitokea kila mwaka nchini Sudan, athari zinatarajiwa kuwa mbaya zaidi mwaka huu baada ya zaidi ya miezi 16 ya mapigano kati ya majenerali wapinzani, ambayo yamesukuma mamilioni ya watu waliokimbia makazi yao.

Pia, wizara hiyo ilielezwa kuwa takribani nyumba 12,420 zimebomoka kabisa na nyingine 11,472 zimeharibika kwa wastani kutokana na mvua hiyo, na kwamba uharibifu mkubwa uko katika majimbo ya Kaskazini na Mto Nile.

Ilielezwa kuwa, mvua kubwa ilifurika juzi eneo la Arbaat Kaskazini mwa mji wa Bahari Nyekundu wa Port Sudan, na kusababisha Bwawa la Arbaat kuporomoka na kusomba vijiji.

"Mto huo ulisomba nyumba na wanyama; watu walipanda milimani ili kujilinda," Issa Adroub mkazi wa eneo hilo alisema.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa bwawa hilo ni chanzo muhimu cha maji kwa Mji wa Port Sudan, ambako maofisa walihamishiwa baada ya vita kuzuka mjini Khartoum.

Wafanyakazi wa kujitolea wa eneo hilo wanaosaidia katika juhudi za kutoa misaada waliiambia AFP kwamba watu 13 wamepatikana wamekufa, wakiwamo wanawake na watoto, na msako unaendelea kuwatafuta watu 210 waliopotea." **TRT**

# Wanaopinga mradi wa mafuta nchini Uganda wakamatwa

**KAMPALA,** Uganda

POLISI nchini Uganda imewakamata wanaharakati 21 wa kutetea mazingira katika mji mkuu Kampala walipokuwa wakiandamana kupinga mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) ambao umeelezwa unagharimu mabilioni ya dola.

Mmoja wa mawakili wa wanaharakati hao wa mazingira Samuel Wanda, alisema watu 21 waliokamatwa ni wanaume 19 na wanawake wawili ambao walijaribu kuandamana kuelekea bungeni na ofisi ya ubalozi wa China.

Mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), unaoongozwa na kampuni kubwa ya mafuta ya Ufaransa ya TotalEnergies, unahusisha uchimbaji wa mafuta nchini Uganda na kusafarisha mafuta ghafi hadi Tanzania kwa ajili ya mauzo ya nje.

Mradi huo utakaokuwa na uwezo wa kuvuna hadi mapipa bilioni 1.7 ya mafuta ghafi, una urefu wa jumla ya kilomita 1443 kati ya hizo 296 zipo Uganda na 1147 Tanzania ambako bomba linapita katika mikoa nane ya Tanzania, mahalani Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga.

Wanaharakati wa kutetea mazingira wanaeleza kuwa, mradi huo una athari mbaya kwa jamii na mazingira kwa kuwa shughuli ya uchimbaji inafanyika katika hifadhi ya kitaifa ya Murchison Falls, ambalo ni eneo kubwa lililohifadhiwa nchini Uganda.

Kampuni inayoongoza bomba hilo imejitetea ikisema kwamba watu waliopoteza makaazi yao au kuathirika kutokana na mradi huo wamelipwa fidia na kwamba hatua zimechukuliwa ili kulinda mazingira.

Wanda alieleza kuwa, wanaharakati wanane kati ya waliokamatwa wangeathirika moja kwa moja na mradi huo, na kwamba walikuwa wanashikiliwa katika kituo cha polisi cha Kampala lakini maofisa usalama bado hawajafafanua mashtaka dhidi yao.

Katika shauri lililoonekana katika shirika la habari la AFP, waandamanaji hao walitoa ombi la dharura dhidi ya kile walichokiita ukiukaji unaoendelea wa haki za binadamu na uchafuzi wa mazingira unaofanywa na mradi wa EACOP.

Shauri hilo lilieleza kuwa, mradi huo wa mafuta ni tishio kwa uchumi wa ndani ya Uganda na kwamba una athari hasi za kijamii na kitamaduni.

Gharama za kukamilisha ujenzi wa mradi wa bomba zinatarajiwa kufikia takribani Sh. Trilioni 8, ikielezwa kuwa bomba hilo litajengwa na kuendeshwa pia na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), kampuni ya CNOOC ya China kwa ubia na kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC).

Hata hivyo, ilielezwa kuwa mafuta ya kwanza yanatarajiwa kusafirishwa 2025, na mradi huo umepongezwa na Rais Yoweri Museveni kama faida ya kiuchumi kwa nchi hiyo isiyo na bandari na ambayo watu wengi wanaishi katika umaskini.

**DW**




Maofisa wa polisi wa Uganda wakimkamata mwanaharakati wa mazingira mbele ya Bunge la Uganda wakati wa maandamano dhidi ya bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) mjini Kampala. **PICHA: MTANDAO**.

# Russia yaishambulia tena Ukraine

**KYIV,** Ukraine

RUSSIA imeilenga Ukraine kwa wimbi jingine la mashambulizi ya usiku kucha na kusababisha vifo vya watu wanne na pamoja na uharibifu wa miundombini pamoja na makazi ya wananchi.

Ilielezwa kuwa, mashambulizi hayo yalifanyika usiku wa kuamkia jana, na kwamba tahadhari za uvamizi wa anga zilitolewa mapema asubuhi, wakati wachunguzi wa Ukraine wapogundua ndege ya Kirussia ikirusha kombora la hypersonic.

Mkuu wa Mkoa wa Zaporizhzhia Ivan Fedorov, alisema mtu mmoja aliuawa na wengine kujeruhiwa katika mji huo, huku milipuko ikiripotiwa kutokea pia katika mikoa ya Kyiv, Sumy, Khmelnytsky na Mykolayiv.

Mashambulizi hayo yanajiri siku moja baada ya Russia kuishambulia Ukraine kwa mojawapo ya mashambulizi makubwa zaidi ya anga katika vita hivyo, na kujeruhi makumi ya watu, huku umeme ukikatika katika miji mingi. Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky aliapa kuwa Kyiv italipiza kisasi baada ya nchi hiyo kukumbwa na duru nyingine ya mashambulizi ya Russia, akieleza kuwa shughuli za uokoaji zinaendelea, lakini watu wanne wameuawa na wengine 16 kujeruhiwa katika mashambulizi hayo.

Ilielezwa kuwa, Russia ilishambulia zaidi ya shabaha 90 za angani dhidi ya raia na miundombinu, zikiwamo ndege zisizo na rubani 81, na makombora ya masafa marefu ya balestiki na ya kurushwa angani.

"Bila shaka tutaijibu Russia kwa mashambulizi haya na mengine yote. Uhalifu dhidi ya binadamu hauwezi kwenda bila kuadhibiwa," Zelensky alisema katika chapisho kwenye mtandao wa kijamii.

Naye, Rais wa Marekani Joe Biden alilaani shambulizi hilo akisema Moscow haitafanikiwa katika vita vyake vinavyoendelea, na kwamba Washington itaendelea kuunga mkono gridi ya nishati ya Ukraine.

"Ninalaani, kwa nguvu zote, kuendelea kwa vita vya Russia dhidi ya Ukraine na juhudi zake za kuwatumbukiza gizani watu wa Ukraine, Russia haitafanikiwa kamwe nchini Ukraine, na roho ya watu wa Ukraine haitavunjika kamwe," Biden alisema katika chapisho kwenye X.

Wakati huohuo Rais wa Ukraine anaiomba Uingereza, Marekani na washirika wengine kutoa idhini kwa Ukraine kutumia silaha zilizotengenezwa na nchi za Magharibi, za masafa marefu kushambulia maghala ya risasi, ndege na viwanja vya ndege ndani kabisa ya Russia.

**BBC**

# MANARA: WACHEZAJI SULUHISHO NYONGA, MAGOTI NI MLOGANZILA

**Na Christina Mwakangale**

MCHEZAJI wa zamani wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Sunday Manara, amewataka wachezaji wenzake wenye tatizo la nyonga na magoti, wasisite kufika katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)- Mloganzila, kupata matibabu.

Manara, ambaye ni miongoni mwa wagonjwa 173 waliopatiwa matibabu hayo hospitalini hapo, aliyasema hayo Dar es Salaam juzi, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kambi ya upasuaji na upandikizaji wa nyonga na magoti.

MNH-Mloganzila, inawafanyia upasuaji na upandikizaji wa nyonga na magoti wagonjwa 30 katika kambi maalum ya siku tano, iliyoanza Agosti 26, mwaka huu.

"Kwa wale Watanzania wenzangu ikiwamo wachezaji kama mimi wenye matatizo ya nyonga au magoti, wasisite kuja Mloganzila kupata huduma hizi, huduma zinazotolewa hapa ni bora sana kwa ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati

"Watanzania wanapopata tatizo la nyonga na magoti wasisite kutibiwa nchini na katika hospitali hii, kwa kuwa kuna wataalam. Huduma zinazotolewa hapa ni bora sana na tuziamini.

"Nina miaka 72 na ninajitahidi kuzingatia masharti na uzito usizidi na nisijitoneshe, MNH ina huduma nzuri. Wanamichezo wanaopata tatizo ni vema kuja kuonana na madaktari kuliko kukata tamaa. Mimi nimefanyiwa na kwa sasa naendelea vizuri na najiona kama nimepona kabisa," alisema Manara.

Manara, alifanyiwa upasuaji na kupandikizwa magoti miezi miwili iliyopita, akisema kwamba kwa sasa anaendelea vizuri, akifanya mazoezi na kufuata ushauri aliopewa na wataalam.

Hospitali hiyo ilianza rasmi matibabu ya upasuaji na upandikizaji wa nyonga na magoti, mwaka 2022 na imeshawafanyia huduma hiyo wagonjwa 173.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, Prof. Mohamed Janabi, alisema kuna ongezeko la tatizo hilo hasa kwa vijana.

"Nchini wamefanyiwa wengi, akiwamo Manara aliyewahi kucheza timu ya Yanga na nyinginezo. Sasa anaona matokeo ya upasuaji huo.

"Duniani upasuaji huu si kitu kigeni na kipya, wamefanyiwa watu maarufu na wanaendelea na maisha yao kama kawaida. Mcheza filamu Arnold Schwarzenegger, mwanamuziki Lionel Richie, walifanyiwa pia upasuaji wa magoti yote," alisema Prof. Janabi.




Mchezaji wa zamani wa Yanga na Taifa Stars, Sunday Manara, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam juzi, kuhusu maendeleo yake baada ya kufanyiwa upasuaji na upandikizaji wa magoti katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)- Mloganzila. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# KMC yaihofia Coastal kesho

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kesho ikitarajia kucheza mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara, KMC FC, imesema inakwenda kucheza na timu ngumu ya Coastal Union, ambayo imetoka kucheza mechi ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, hivyo utakuwa mgumu kwao.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Khalid Chukuchuku, amesema Coastal si timu ya kubeza kwani ndiyo iliyoizuia msimu uliopita kutwaa nafasi ya nne na kucheza mechi za kimataifa.

KMC itakuwa kwenye uwanja wake wa nyumbani, KMC Complex uliopo Mwenge, Dar es Salaam, kucheza mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu dhidi ya Coastal Union.

Mchezo ulipangwa kuchezwa kesho kutokana na ushiriki wa Coastal Union hatua ya awali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola, ambapo tayari imetolewa kwa jumla ya mabao 3-0, ikichapwa idadi hiyo ugenini na kulazimishwa suluhu nyumbani.

Hivyo, mechi hiyo itakuwa ni ya kwanza msimu huu kwenye Ligi Kuu kwa timu zote mbili.

"Najua mchezo utakuwa mgumu kwa sababu si timu ya kubeza, unajua ndiyo timu ambayo msimu uliopita ilituzuia sisi kupanda ndege kwenda kucheza mechi za kimataifa, tuna imani bado msimu huu ni wazuri licha ya kutofanya vema kimataifa, nimemuona kocha Ngawina Ngawina pale," alisema.

Msimu uliopita, Coastal ilimaliza nafasi ya nne, ambayo iliipa tiketi ya kucheza mechi za kimataifa, huku KMC ikishika nafasi ya tano.

Hata hivyo, pamoja na hofu yao na kuwaheshimu Coastal, lakini hawatoenda kinyonge kwani wanaamini wachezaji wao na usajili walioufanya.

"Pamoja na hayo sisi tunajiangalia wenyewe, tunakwenda kupambana nao tuna wachezaji tuliowasajili msimu uliopita na wapya, muunganiko umeshapatikana kilichobaki ni kwenda kuwakabili, tunaamini Alhamisi pale Mwenge watu watakaokuja kuangalia mpira watafurahia sana," alisema Chukuchuku.

## KVZ FC yaanza kazi na safu ya ulinzi, ushambuliaji

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya KVZ FC inaendelea kujifua vema kwa kucheza michezo ya kirafiki kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar utakaoanza kutimua vumbi mwezi ujao huku benchi la ufundi la timu hiyo likielekeza nguvu zaidi katika safu ya ulinzi na ushambuliaji.

Katika michezo minne ambayo KVZ FC mpaka sasa imecheza imefumania nyavu mara saba na kuruhusu nyavu zake kutikiswa mara mbili tu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa timu hiyo, Abdul-jalili Mohmed, alisema timu hiyo inaendelea na mpango wake wa mazoezi kwa mujibu wa ratiba za mwalimu pamoja na kucheza michezo ya kirafiki.

Alisema kupitia michezo ya kirafiki waliyocheza kiwango cha wachezaji kimeendelea kuimarika kwa mujibu wa maelekezo wanayopata kutoka kwa mwalimu wao.

Mohamed alisema wachezaji wameonesha kuyaelewa maelekezo ya mwalimu wao kwa kuona mabadiliko gani yanahitajika kuelekea msimu mpya ili kuwa na mafanikio.

Alisema awali shida ilikuwa katika idara ya umaliziaji jambo ambalo washambuliaji wamefanikiwa kuelewa somo hilo kutokana na mabadiliko wanayoyaonesha katika michezo ya kirafiki waliyocheza.

Ofisa Habari huyo alisema mpango wa pili ambao anaendelea nao ni kuwajenga walinzi ili kuhakikisha wanajenga ngome imara kwa wachezaji wa nafasi hiyo.

"Ili kuwa na kikosi kizuri lazima upate wachezaji ambao watacheza vema katika nafasi zao, na mwalimu ameanza kwa nafasi hizo muhimu ambazo ndio zitakazotoa mafanikio," alisema.

Hata hivyo, alisema wanasubiri ratiba kutoka Bodi ya Ligi Zanzibar ili kuangalia uwezekano wa kuweka kambi ya wiki moja kabla ya msimu kuanza.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### OSIMHEN AITAKA CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa Napoli na Timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25, angependelea kuhamia Chelsea tofauti na tetesi zinazomhusisha na klabu moja nchini Saudi Arabia. (***i***)

### RAHEEM TAYARI KUTUA UTD

WINGA wa England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 29, yuko tayari kuhamia Manchester United, lakini hataendelea na uhamisho hadi atakapojadili zaidi mkataba wake na Chelsea. (***Telegraph***)

### NKETIAH AKARIBIA PALACE

KLABU ya Crystal Palace inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili mshambuliaji wa Arsenal na England, Eddie Nketiah mwenye umri wa miaka 25, kwa pauni milioni 25, pamoja na nyongeza za pauni milioni tano. (***Athletic***)

### EDOUARD ATAKIWA CELTIC

MABINGWA wa Scotland, Celtic wana nia ya kumsajili tena mshambuliaji Mfaransa Odsonne Edouard mwenye umri wa miaka 26, kutoka Crystal Palace. (***News Shoppers***)

### NUNES KWA MKOPO

KLABU ya Atletico Madrid inatathmini uwezekano wa kumsajili kwa mkopo kiungo wa kati wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Ureno, Matheus Nunes, ingawa bado hawajawasilisha ombi. (***Athletic***)

### MAMADASHVILI KUBAKI

KIPA wa Georgia, Giorgi Mamadashvili, alifanyiwa vipimo vya afya nchini Hispania siku ya Jumatatu alipokuwa anakamilisha uhamisho wa pauni milioni 30 kwenda Liverpool. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, atasalia Valencia na kuhamia Merseyside msimu wa majira ya joto wa 2025. (***Times***)

### JAMES ATAJWA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest wanapanga kumnunua kiungo wa kati wa Uingereza James Ward-Prowse mwenye miaka 29, ambaye hayupo katika mipango ya kocha mpya wa West Ham, Julen Lopetegui. (***Football Insider***)

### WEST HAM HAITAKI KUUZA

KLABU ya West Ham wako tayari kupokea ofa kwa ajili ya James Ward-Prowse, lakini hawana nia ya kumuuza. (***Sky Sports***)

### TRAFFORD ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle wamerejea tena katika jaribio la kumsajili mlinda lango wa Burnley na timu ya England chini ya umri wa miaka 21, James Trafford, huku mkataba wa mkopo unaotarajiwa na wajibu wa kumnunua ukijadiliwa. (***Guardian***)

### KAYODE AIVUTIA BRENTFORD

KLABU ya Brentford wanavutiwa na beki wa Fiorentina ya Italia, Michael Kayode mwenye umri wa miaka 20, ambaye pia anawaniwa na klabu kadhaa. (***Sky Sports***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# OLMO ACHUKUA NAFASI YA CHRISTENSEN BARCA

**BARCELONA,** Hispania

## ●●● Ni kutokana na jeraha la muda mrefu alilopata, LaLiga yaikubalia baada ya...

HATIMAYE Dani Olmo jana alikuwa tayari kucheza mechi yake ya kwanza kwa Barcelona dhidi ya Rayo Vallecano baada ya usajili wa muda kuidhinishwa na LaLiga, vyanzo vimethibitisha kwa ESPN.

Olmo, aliyewasili kwa Euro milioni 55 kutoka RB Leipzig, amekosa mechi mbili za kwanza za Barca msimu huu kwa sababu usajili wake haukushughulikiwa na LaLiga kutokana na klabu kuendelea kuwa na matatizo ya kifedha.

**Vyanzo viliiambia ESPN jana kwamba jeraha la muda mrefu alilopata Andreas Christensen litatoa nafasi ya kusajili nyongeza mpya.**

Kifungu cha 77 cha Kanuni za Maandalizi ya Bajeti ya LaLiga kinaruhusu klabu kuvuka kiwango cha matumizi yao endapo mchezaji kwenye kikosi atakabiliwa na majeraha ya muda mrefu.

Barca wametuma ripoti za kimatibabu kwa LaLiga ikieleza kwamba tatizo la kifundo cha mguu litamweka nje Christensen hadi miezi minne, na kuwaruhusu kutumia asilimia 80 ya mshahara wa beki huyo wa kati wa Denmark kusajili mchezaji mwingine kwa wakati huo.

Vyanzo vimethibitisha hilo liliipa Barca nafasi ya kutosha kumsajili Olmo kabla ya mechi ya jana.

Barca ilikuwa imeanza kufanya harakati za kumsajili Olmo kwa mfululizo wa kuondoka, Ilkay Gundogan, Vitor Roque, Mika Faye na Clement Lenglet ni miongoni mwa wale ambao wameihama klabu hiyo wiki iliyopita, ingawa haikutosha kumsajili Olmo.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Hispania, ambaye alichezea akademi ya Barca hadi alipokuwa na umri wa miaka 16 kabla ya kwenda Croatia, ataruhusiwa kusajiliwa hadi Desemba 31.

Chanzo kimoja kinasema Barca wanatumaini kuwa itadhibitisha hatua ya muda na kwamba biashara yao kabla ya mwisho wa dirisha la uhamisho pia itawaruhusu kuwa na Christensen na Olmo wote waliosajiliwa ipasavyo kabla ya Januari.

Si mara ya kwanza kwa Barca kujirudia katika Kifungu cha 77 kusajili wachezaji.

Walitumia fomula sawa msimu wa baridi uliopita na Vitor Roque, wakitumia jeraha la Gavi kulazimisha kwa muda kupitia usajili wa mshambuliaji huyo wa Brazil, ambaye alijiunga na Real Betis kwa mkopo Jumatatu.

Barca pia walitumia Kifungu cha 77 mapema mwezi huu kuhakikisha beki wa kati Inigo Martinez amesajiliwa kwa ajili ya kuanza kwa msimu huu, huku Ronald Araujo akiwa mchezaji aliyejeruhiwa ambaye nafasi yake ya mshahara inaweza kutumika.

HABARI MICHEZO




# CHELSEA WAJITOSA USAJILI WA SANCHO

**LONDON,** England

CHELSEA inafikiria kushindana na Juventus kwa ajili ya kumsajili Jadon Sancho, chanzo kiliiambia ESPN.

Manchester United iko tayari kumruhusu mshambuliaji huyo kuondoka kabla ya tarehe ya mwisho ya kuhama Ijumaa.

Juventus imefanya mazungumzo na United, lakini hadi sasa makubaliano hayajafikiwa.

Sancho, kwa mujibu wa chanzo, ni miongoni mwa chaguzi kadhaa ambazo Chelsea inawaza katika wiki ya mwisho ya dirisha.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, bado hajaichezea United hadi sasa msimu huu baada ya kuondolewa kwenye kikosi kilichocheza dhidi ya Fulham na Brighton.

Amerudishwa Old Trafford msimu huu wa majira ya joto baada ya kutumia kipindi cha pili cha msimu uliopita kwa mkopo katika Klabu ya Borussia Dortmund.

Sancho aliingia kama mchezaji wa akiba katika mechi ya kipigo cha Ngao ya Jamii dhidi ya Manchester City, lakini hajacheza mchezo wa ushindani kwa United kwa mwaka mmoja kutokana na kutofautiana kwake hadharani na kocha, Erik ten Hag mnamo Agosti 2023.

United ingependelea kupata uhamisho wa kudumu kwa Sancho, lakini hadi sasa klabu zimekuwa haziko tayari kufikia thamani ya karibu pauni milioni 40.

Mshahara wa Sancho wa zaidi ya pauni 300,000 kwa wiki pia ni kikwazo.

Amebakiza miaka miwili kwenye mkataba uliosaini alipowasili kutoka Dortmund kwa mkataba wa pauni milioni 73 mwaka 2021.

United haijakataa kukubaliana na mkataba wa awali wa mkopo kwa Sancho, mradi tu kuna chaguo au wajibu wa kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu mwishoni mwa kampeni.

# Ugarte rasmi mali ya Man United

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imekubali kufikia makubaliano ya kimkataba na Paris Saint-Germain kwa ajili ya kumsajili kiungo Manuel Ugarte, kwa mujibu wa ESPN.




United wamefikia makubaliano juu ya mkataba wenye thamani ya pauni milioni 42 na pauni milioni 8 za nyongeza zinazowezekana.

Ugarte jana alisafiri kwenda Manchester kufanyiwa vipimo vya afya na kukamilisha rasmi uhamisho huo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, anaweza kucheza mechi yake ya kwanza dhidi ya Liverpool katika Uwanja wa Old Trafford Jumapili, kulingana na kibali cha kimataifa.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Uruguay amekuwa akilengwa na United kwenye safu ya kiungo msimu huu na anachukua matumizi ya United wakati wa dirisha la majira haya ya kiangazi hadi kufikia zaidi ya euro milioni 180.

Klabu hiyo inatarajia kupata kitita kingine cha fedha kwa kumruhusu Scott McTominay kujiunga na Napoli.

Man United imekubali ada ya pauni milioni 25 na timu hiyo ya Italia na wamempa ruhusa McTominay kujadiliana nao maslahi binafsi.

Kwa mujibu wa ESPN, mchezaji huyo wa Kimataifa wa Scotland jana alitarajiwa kusafiri kwa ajili ya uchunguzi wa kiafya.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Ugarte aliweka wazi kwa PSG kwamba anataka kuhamia United na aliachwa nje ya mechi zao mbili za kwanza za Ligue 1 msimu mpya dhidi ya Le Havre na Montpellier.

Alicheza mechi 37 katika michuano yote akiwa na PSG msimu uliopita baada ya kuwasili kutoka Sporting CP kwa uhamisho wa pauni milioni 50 mwaka 2023.

United wanatazamiwa kuidhinisha wachezaji zaidi wanaoondoka kabla ya tarehe ya mwisho ya uhamisho Ijumaa.

Kiungo Hannibal Mejbri atajiunga na Klabu ya Championship Burnley baada ya kufanyiwa uchunguzi wa kiafya Jumatatu.

Klabu hiyo pia inatazamia kumtoa mlinzi Victor Lindelof, ingawa hatua hiyo imekuwa ngumu kutokana na mchezaji huyo wa Kimataifa wa Sweden kupata jeraha la kidole cha mguu ambalo limemfanya kuwa nje ya uwanja.

## Liverpool yamuibukia Federico Chiesa

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL inafikiria kumnunua Federico Chiesa kabla ya tarehe ya mwisho ya uhamisho Ijumaa baada ya kufahamishwa kuhusu kupatikana kwa mshambuliaji huyo wa Juventus, chanzo kiliiambia ESPN.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, alikuwa karibu na uhamisho wa Euro milioni 13 kwenda Barcelona mapema mwezi huu, lakini klabu hiyo ya LaLiga imeshindwa kupanga makubaliano na sasa Liverpool inafanya uchunguzi wa kina juu ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia.

Chiesa, ambaye mkataba wake na Juventus unamalizika mwishoni mwa msimu huu, amekumbwa na majeraha kadhaa, ikiwa ni pamoja na kuachwa nje kwa miezi 10, tangu alipoisaidia timu ya Roberto Mancini ya Italia kupata mafanikio katika michuano ya Euro 2020.

Lakini licha ya rekodi yake ya utimamu wa hali ya juu, Liverpool inavutiwa na Chiesa kutokana na uhodari wake.

Liverpool bado haijafanya usajili msimu huu wa majira ya joto kutokana na kuteuliwa kwa Arne Slot kama kocha mkuu baada ya Jurgen Klopp kuondoka Anfield mwishoni mwa msimu uliopita.

Mazungumzo yanaendelea kuhusu dili la euro milioni 40 kwa mlinda mlango wa Valencia Giorgi Mamadashvili - mkataba ambao utamfanya mchezaji huyo wa Kimataifa wa Georgia kusalia katika klabu hiyo ya Hispania kwa mkopo kwa muda uliosalia wa msimu huu.

Lakini wakati Slot amesema kuwa anafuraha na kikosi chake kilichopo, Liverpool bado inaweza kumuongeza Chiesa wiki hii ikiwa dili linalofaa linaweza kufikiwa na Juventus.



# Azam FC warejea kisaikolojia kuivaa JKT

**Na Shufaa Lyimo**

LICHA ya kueleza kwamba wachezaji wake walivurugwa kisaikolojia baada ya kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na APR ya Rwanda, Kocha Mkuu wa Azam FC, Bruno Ferry, amesema hali kwa sasa si mbaya na wapo tayari kuivaa JKT Tanzania kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara leo.

JKT Tanzania itaikaribisha Azam FC katika mechi ya Ligi Kuu Bara, itakayopigwa majira ya saa 10 jioni kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo uliopo Mbweni, Dar es Salaam.

Azam itashuka dimbani ikiwa imetoka kutolewa kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na APR kwa jumla ya mabao 2-1 baada ya wiki iliyopita Wanyarwanda hao kupindua matokeo ya kuchapwa bao 1-0 Dar es Salaam kwa kuibuka na ushindi wa mabao 2-0.

Kuelekea mchezo huo, jana Kocha Mkuu wa Azam FC, Ferry alisema baada ya kutolewa kwenye mashindano hayo saikolojia za wachezaji zilivurugika kwa kiasi kikubwa.

"Baada ya kuondolewa kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa wachezaji wangu hawakuwa vizuri kisaikolojia, nilikaa na kuzungumza nao ili niwaweke sawa kwa ajili ya kujipanga na michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema Ferry. Alisema kwa sasa wako sawa na wanaelekeza nguvu zao kwenye mashindano ya Ligi Kuu Tanzania Bara wakianzia na mchezo wa leo.

Aidha, Ferry alisema wachezaji ambao hawakuwapo kwa kipindi kirefu kutokana na kuwa majeruhi, bado wataendelea kukosekana mpaka hapo watakapokuwa sawa kiafya.

Naye mchezaji wa timu hiyo, Hamis Yassin, ambaye alizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake, alisema baada ya kuotolewa na APR hawakuwa sawa kwani hawakuyatarajia matokeo waliyoyapata, lakini sasa wapo tayari kwa Ligi Kuu.

"Mchezo huo utakuwa mgumu na wenye upinzani mkubwa kutokana na aina ya timu tunayokwenda kukutana nayo, yaliyotokea yamepita tunaelekeza nguvu zetu katika mchezo huo," alisema Yasini.

Kwa upande wa Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zakaria ,Zaka Zakazi alisema wamejipanga vizuri na kudai bado wataendelea kuwapo na kocha wao mkuu.

Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Hamad Ally, alisema wataingia kwa tahadhari katika mchezo huo kwa kuwa wanakutana na timu ambayo ina ubora mkubwa.

"Tunafahamu Azam FC ni timu nzuri, hivyo tutaingia kwa tahadhari kubwa kwa kutambua wamekamilika idara zote ili tuweze kupata pointi tatu," alisema Ally.

Hassan Dilunga ambaye alizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake wa JKT Tanzania, alisema wamejipanga vizuri licha ya kutarajia mchezo huo kuwa mgumu na wenye upinzani mkubwa.

"Tunafahamu mchezo utakuwa mgumu lakini tutapambana kuhakikisha tunapata ushindi kwenye uwanja wetu wa nyumbani," alisema Dilunga.

# SIMBA, YANGA ZAWAITA WATANZANIA KUSHUHUDIA MASHINDANO YA QURAN

**Na Waandishi Wetu**

KLABU za Simba, Yanga pamoja na Azam FC zimewataka Watanzania kujitokeza kwa wingi katika mashindano ya Dunia ya Quran Tukufu kwa wasichana yatakayofanyika Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Hassan Suluhu.

Wakizungumza katika mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kwa upande wa Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, alianza kwa kuwapongeza viongozi wa dini kuandaa mashindano hayo ya kushindana kusoma kitabu cha Mwenyezi Mungu.

"Tunatambua thamani ya mwanamke katika jamii, ninaomba Watanzania wajitokeze kwa wingi siku hiyo kuwaunga mkono dada zetu ambao watakuwa wanashindana kusoma kitabu cha kumtukuza Mungu," alisema Ahmed.

Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, alisema watashirikiana na viongozi hao wa dini kuhakikisha tukio hilo linafanyika kama lilivyopangwa.

"Ni bahati kubwa rais wetu kushuhudia tukio kubwa kama hilo ambalo linakwenda kufanywa na wanawake kutukuza neno la Mungu, ninaomba Watanzania waje kwa wingi siku hiyo," alisema Kamwe.

Msemaji wa Azam FC, Hashimu Ibwe, alisema mpira wa miguu ni mchezo wa furaha, mazoezi na hauhusiani na uadui, ndio maana kwa pamoja wameunganishwa na BAKWATA katika kulisemea shindano la wanawake la kusoma na kuhifadhi Quran, Jumamosi ya Agosti 31.

"Isingekuwa mchezo wa mpira tusingejumuishwa kwa pamoja na viongozi wa dini wakubwa kwa lengo la kufanikisha mashindano haya, ambapo nasi kama Azam tunafurahia kuwapo hapa sambamba na kuguswa na mgeni rasmi, Dk. Samia Jumamosi," alisema Ibwe.

Kwa mujibu wa BAKWATA, shindano hilo linatambua umuhimu wa michezo, hali iliyowalazimu kuwaalika wasemaji wa klabu kubwa za mpira wa miguu Tanzania, kushiriki katika kuhamasisha wafuasi wao wahudhurie kwa wingi kwenye shindano hilo la kimataifa ambalo halitakuwa na kiingilio.

Aidha, Mufti Mkuu wa Tanzania, Abubakari Zuber, alisema mashindano hayo yatashirikisha mataifa 12 na kwamba siku hiyo utazinduliwa msaafu mpya wa kielektroniki.

"Siku hiyo kutakuwa na matukio mbalimbali likiwamo lile la utoaji wa tuzo vile vile yatahudhuriwa na viongozi wengi wa dini kutoka mataifa mbalimbali," alisema Zuber.

Kwa upande wa Shehe Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa, alisema jambo hilo ni la aina yake kwani Rais Samia ndiye atakuwa wa kwanza kushuhudia mashindano makubwa ya Quran.

# Simba, Al Hilal kukiwasha Dar, Camara, Mukwala...

INATOKA UK. 24

robo fainali, nyinyi mnatakiwa mvuke zaidi ya hapo na ndicho kilichosababisha majiliwe Simba," alisema Ahmed.

Simba, ambayo ni moja kati ya timu chache Afrika kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho zilizopita moja kwa moja raundi ya kwanza, itaanza mechi yake ya kwanza, Septemba 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa Juni 11, nchini Libya dhidi ya timu hiyo, kabla ya kurudiana, Septemba 20, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Wakati huo huo, wachezaji wapya watatu wa timu hiyo, wameitwa kwenye vikosi vyao vya timu ya taifa kujiandaa na michezo ya kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2025, zinazotarajiwa kuchezwa mwakani nchini Morocco.

Straika Mukwala, aliyesaliwa msimu huu, ameitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Uganda (The Cranes), ambacho kiko Kundi K, kikijiandaa na mechi dhidi ya Afrika Kusini, Septemba 6, ikiwa ugenini, golikipa Camara akiwa ameteuliwa kuunda kikosi cha Timu ya Taifa ya Guinea kilichopo Kundi H pamoja na Timu ya Taifa ya Tanzania, kitakuwa ugenini dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Septemba 6, mwaka huu.

Mwingine ni beki wa kushoto, ambaye, Nouma, akienda kuunda kikosi cha Burkina Faso ambacho siku hiyo hiyo kitakuwa ugenini dhidi ya Senegal, ukiwa ni mchezo wa Kundi L.

Wachezaji wengine watatu wa Tanzania wa timu hiyo, Ali Salim, Mohamed Hussein ,Tshabalala' na Edwin Balua, wapo kwenye kikosi cha Taifa Stars kinachotarajia kucheza dhidi ya Ethiopia, Septemba 4, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema licha ya ushindi walioupata kwenye michezo miwili ya Ligi Kuu Tanzania Bara, bado kikosi chake hakijaanza kucheza soka analolitaka.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Fadlu, alisema anaendelea kuingiza mbinu na mifumo yake kwenye timu na anaamini baada ya muda mchache timu hiyo itakuwa moto.

"Nafurahi tumepata ushindi kwenye michezo yetu miwili iliyopita, lakini kwangu bado sijaridhika na kile ninachokitaka, Simba ina nafasi ya kucheza soka la juu zaidi, naamini baada ya muda kikosi kitakuwa na mabadiliko makubwa," alisema Fadlu.

Alisema anaendelea kukiimarisha kikosi na anaridhishwa na kile wanachokifanya wachezaji wake kwenye uwanja wa mazoezi.

"Napenda namna wachezaji wanavyopambana kutafuta namba, ni kitu ambacho nakipenda kwenye kikosi changu, hii itaongeza hali ya kupambana, kwa sasa kazi kubwa kwangu ni kuingiza mfumo na mbinu zangu taratibu, baada ya muda mfupi Simba itacheza mpira mzuri zaidi ya huu," alisema Fadlu.

Alisema anataka kuona kila mchezaji anayepata nafasi ya



Moussa Camara

kucheza anasaidia timu na kutengeneza kikosi kipana.

"Nataka atakayekuwa ndani ni sawa na yule atakayekuwa kwenye benchi, kila mchezaji nataka awe anapata nafasi kulingana na aina ya mfumo nitakaotumia na aina ya mpinzani wetu," alisema Fadlu.

Katika hatua nyingine, kikosi cha Simba kinatarajia kucheza mchezo wa kirafiki Jumamosi dhidi ya Al Hilal ya Sudan ikiwa ni sehemu ya maandalizi yao kabla ya kuanza kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Timu hizo zote zinatarajia kushiriki mashindano ya Afrika na mchezo huo ni sehemu ya maandalizi yao kabla ya michezo yao ya CAF.

Kocha wa simba, Fadlu, alisema mchezo huo ni kipimo kizuri kwao kuelekea kwenye mchezo wao wa mzunguko wa kwanza hatua ya kwanza dhidi ya Al Ahly Tripoli ya Libya.

Simba itaanza kampeni yake kwenye mashindano hayo ya CAF kwa kuanzia ugenini Septemba 13 kabla yakurudiana jijini Dar es Salaam wiki moja baadae ili kusaka nafasi ya kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo.

# Michezo



Nipashe

Jumatano Agosti 28, 2024


**Chelsea wajitosa usajili wa Sancho**

UKURASA 22



Wachezaji wa Yanga, Clement Mzize, akiwa katika himaya ya kumiliki mpira mazoezini dhidi ya Nickson Kibabage. Huduma ya Mzize inawaniwa na klabu kadhaa Afrika na Ulaya. **PICHA: MAKTABA**

## Simba, Al Hilal kukiwasha Dar

- Mukwala, Camara, Nouma waitwa timu zao za taifa

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

WAKATI wachezaji wake, Steven Mukwala, Moussa Camara na Valentin Nouma, wakiitwa kwenye timu zao za taifa, Klabu ya Simba inatarajiwa kucheza mechi ya kujipima nguvu nchini dhidi Al Hilal ya Sudan Jumamosi wiki hii, kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wake wa raundi ya kwanza Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Ahly Tripoli ya Libya, huku wakiweka malengo yao ni kufika hatua ya nusu fainali.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema tayari wameshakaa na wachezaji wao na kuwaeleza malengo hayo, licha ya kwamba kikosi chao kina wachezaji wengi wapya.

Alisema pamoja na upya wao, lakini Klabu ya Simba haiwezi kuondoka nje ya malengo yake iliyojiwekea.

"Kwa sasa wachezaji wapo mapumziko, lakini watarejea mazoezini, tutakuwa na michezo kadhaa ya kirafiki, ukiwamo dhidi ya Al Hilal ya Sudan, utakuwa mchezo maalum wa wachezaji kupata ladha ya michezo ya kimataifa, lakini baada ya hapo tutaanza rasmi maandalizi ya mchezo wetu dhidi ya Al Ahly Tripoli.

"Tukishamaliza michezo ya kirafiki, benchi la ufundi litatoa tathmini yake ya kitu gani kinahitajika kabla ya mchezo wetu wa Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Najua tuna kikosi kipya, lakini malengo yetu ni makubwa, yapo pale pale, lengo ni hatua ya juu zaidi ya robo fainali, tumeshakaa na wachezaji tumewaambia, wenzenu huwa wanaishia

INAENDELEA UK. 23

# YANGA YAMWEKEA NGUMU MZIZE

- Yasema haiuzi mchezaji yeyote hadi ifike fainali, michuano CAF na kwamba...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema haitouza au kuruhusu mchezaji yeyote tegemeo aondoke kwenye kikosi chake mpaka hapo watakapotimiza lengo lao la kutinga hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kufika fainali au kuutwaa ubingwa wenyewe.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema kinachofanyika kwa sasa ni kutaka kuidhoofisha Yanga kama ambavyo klabu mbalimbali kubwa barani Afrika zimekuwa zikifanya kwa klabu ndogo hasa za Tanzania wanapoona zimekuwa hatari katika michuano ya kimataifa.

Alisema hayo kutokana na kile kilichoonekana klabu hiyo kumzuia straika wao, Clement Mzize, ambaye amekuwa akihitajika na klabu mbalimbali.

Klabu za Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, Wydad Casablanca ya Morocco, Aalborg BK ya Denmark na Crawley Town FC inayocheza Ligi Daraja la Pili Uingereza, zinadaiwa zimepiga hodi Yanga kutaka huduma za mchezaji huyo, lakini hazijajibiwa.

**Taarifa zinaeleza Wydad ndiyo imekuwa ikimhitaji zaidi, kwani imepiga hodi mara tatu na mara zote hizo imekuwa ikizidisha dau la uhamisho, lakini Yanga imekuwa kimya.**

"Jambo hili ngoja nilitolee ufafanuzi, miaka ya nyuma ilionekana wachezaji wazuri kutoka nje hawawezi kucheza ligi yetu ya Tanzania, na ikitokea kwa uchache wao wakishakuwa na uwezo mkubwa, klabu zenye fedha zilikuwa zinakuja kutuchukulia wachezaji na kutudhoofisha, zimekuwa zikiturudisha nyuma katika michuano ya kimataifa, yaani mnafanya vema, wakazoa wale wazuri tegemezi mnaanza upya, inachukua tena misimu miwili au mitatu kukaa sawa.

"Sasa hivi klabu za Tanzania zinaweza kuleta wachezaji wazuri wakacheza Ligi Kuu, na pia sasa zina uchumi mzuri wa kuwazuia na kuwabakisha wachezaji bora, kwa hiyo si Mzize tu, mchezaji yeyote yule tegemeo Yanga haondoki mpaka azma yetu ya kutwaa ubingwa wa Afrika itakapotimia," alisema Kamwe.

Alisema mashabiki wa soka wasilichukulie suala hili upande wa hasi tu kuwa klabu yao ikatakaa kuuza au kuruhusu wachezaji wake, lakini pia wachukue upande wa chanya kwani una faida kubwa, timu yoyote inayotaka kufanya vema katika michezo ya kimataifa haipaswi kuondoa wachezaji wake bora, vinginevyo haitofika popote na kila mwaka itakuwa inashiriki badala ya kushindana.

Kamwe, pia amethibitisha klabu hiyo kuachana na winga wao raia wa Afrika Kusini, Mahlatse ‚Skudu‘ Makudubela.

"Ni sahihi, mazungumzo yetu na Skudu yamefikia tamati, kwa sasa si tena mchezaji wa Yanga, tunamtakiwa kila lakheri," alisema.

Mchezaji huyo alisajiliwa kwa mbwembwe akitokea Marumo Galants ya Afrika Kusini, lakini hakucheza kwa mafanikio.

Wakati huo huo, kikosi cha Yanga kiliondoka jijini Dar es Salaam kwa mafungu juzi na jana kwa ndege, kuelekea mkoani Kagera kwa ajili ya mchezo wa raundi ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara, dhidi ya Kagera Sugar, unaotarajiwa kuchezwa kesho katika Uwanja wa Kaitaba, Bukoba.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >